Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 174 | RAJAB 1434 AH | MEI 2013 | HIJRAT 1392 HS | BEI TSH. 500/=

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

**Anayestawisha misikiti ya Mwenyezi Mungu ni yeye tu amwaminiye Mwenyezi Mungu na Siku ya mwisho, na kusimamisha Sala na kutoa Zaka na hamwogopi ye yote ila Mwenyezi Mungu; basi hao huenda wakawa miongoni mwa walioongozwa.**
**(Taubah - 9:18)**

# 'Nuru ya Ahmadiyya' Yaangaza Vancouver - Canada

**Na Mwandishi wetu**

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. katika ziara yake ya hivi karibuni nchini Canada amefafanua umuhimu na nafasi ya msikiti katika maisha na maendeleo ya Islam. Akifungua msikiti wa Baitul Rahmaan katika jiji la Vancouver, Kiongozi huyo alisema ujenzi wa msikiti mahali popote unafungua milango ya Baraka na unatoa taswira ya uhai wa Islam. Akimnukuu Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., Hadhrat Mirza Masroor Ahmad alisema kujenga msikiti sio tu kwamba kunatangaza umoja wa Mwenyezi Mungu bali pia ni njia ya kuutangaza Uislamu. Akiendelea na ufafanuzi wake, Kiongozi wa Jumuiya ya



*Masjid Baitur Rahman Vancouver Canada uliofunguliwa hivi karibuni*

Ahmadiyya anasema:
Kwa fadhili za Allah baada ya kupita miaka zaidi ya 50 Jamaat katika eneo hili la British Columbia imewezeshwa kujenga msikiti.
Hapo mwanzo kituo au ukumbi ambao wanajumuiya walikusanyika ulikuwepo na hii pengine ndio sababu ya kuchelewa na kutokuona haja ya kujenga msiiti kwa haraka katika eneo hili.
Hata hivyo msikiti unayo nafasi yake malum na zama unapokuwepo sehemu fulani njia mpya za maendeleo na za kuuhubiri Uislam zinafunguka.
Ile hali ya kuwepo jengo la msikiti, mnara wake, kuba lake na sura ya msikiti kunabakisha hisia maalum kwa waumini na hata wakazi wa eneo husika. Hii ndio sababu Masihi Aliyeahidiwa a.s. akatoa kipaumbele maalum kwa ujenzi wa miskiti na akasema kwa kujenga misitiki sio tu kwamba tunatangaza Umoja wa Mungu bali pia njia za kuutangaza Uislam zinafunguka zaidi.
Ni kweli Masihi Aliyeahidiwa a.s amesema haijalishi ukubwa na uzuri wa msikiti bali kinachotakiwa ni kuwa na eneo tu, lakini hii isieleweke kwamba pale penye haja na uwezo tusijenge misikiti mizuri na mikubwa.

Baadhi ya watu wanaweza kudhani kuwa kuna haja gani ya kujenga msikiti mkubwa kama huu wakati ambapo kuna haja kwenye Jumuiya mbalimbali duniani za kujenga misikiti na wakati ambapo wengine hawana uwezo wa kujenga misikiti wao wenyewe na wanahitaji kusaidiwa kutoka Markaz. Hivyo mawazo yanaweza kupita kwamba badala ya kujenga

*Endelea uk. 2*

# Kisa cha Nabii Issa (a.s.) Kusema Uchangani

**Na Mwl. Abdullah H. Mbanga - Dar es Salaam**

Mada tunayoijadili hapa yaweza kuonekana ni tata mno kutokana na dhana za baadhi ya Waislam. Utata huu unatokana na baadhi ya Waislam kufuata itikadi za kubuni wakiamini kuwa itikadi hizo zinaonyesha utukufu, uwezo na miujiza ya Mwenyezi Mungu. Moja wapo ya dhana za aina hii ni ile itikadi ya kwamba Nabii Isa (as) au Yesu alizungumza akiwa mtoto mchanga. Kwa kuamini hivi, wenyewe hudhani kwamba wanatukuza shani ya uwezo wa Allah, lakini wakasahau kuwa itikadi hiyo, inamtukuza Nabii huyo wa Kiisraeli siyo tu juu ya Manabii na wateule wote wa Mungu, bali hata kuliko Mtukufu wa daraja, Mbora wa viumbe, Mwanzilishi Mtukufu wa Islam Hadhrat Muhammad Mustafa (saw).

La ajabu zaidi ni kwamba imani hii inayohubiriwa kwa nguvu na fahari kubwa miongoni mwa Waislam, haitambuliki kwa Wakristo wanaoamini juu ya uungu wa Yesu, na wala haitajwi popote katika maandiko yao matakatifu. Kama ni kweli hili lilitokea katika maisha ya Yesu, bila shaka ungekuwa ni muujiza mkuu ambao ungepaswa kuandikwa kwa herufi kubwa katika vitabu vya Injili.

Bila shaka huu ni mkanganyiko mkubwa uliowakumba baadhi ya Waislam. Huenda ulitokana na kutoelewa hekima za baadhi ya aya za Qur'an Tukufu wanazozirejea katika kutetea dhana hii. Kwa hivi lengo la makala hii ni kujadili kwa kina juu ya aya hizo na kutoa ufafanuzi wenye lengo la kuondoa mkanganyiko huo unaomtukuza Nabii Isa juu ya Mtume Mtukufu wa Islam (s.a.w.).

Dhana hii inahusishwa mno na maelezo yanayopatikana katika sura AI-Imran na sura Mariyam. Katika aya ya (3:47) inadaiwa kuwa Isa atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima. Na katika sura (19:27 - 33) inaelezwa hivi; "Na akamleta kwa watu wake akiwa amembeba. Wakasema

*Endelea uk. 5*

# 'Mtenda Mema' Kwa Mola Katangulia

*Na Mahmood Hamsin Mubiru Dar es Salaam*

Tarehe 10/05/2013 ni siku ambayo ni vigumu kwa ulimwengu wa Kiswahili bilkhususi tanzu ya ushairi kuisahau, kwani ni siku ilipompoteza Sihiyana mtunzi wa vina Mwenyekiti wa chama cha UKUTA Taifa, Kiongozi wa Klabu ya Simba, Mzee wa chama cha Mapinduzi maarufu kwa lakabu ya Mtendamema ambaye alifahamika zaidi kwa jina la Sihiyana Swaleh Omari Mhanuka. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Bwana Sihiyana ambaye jina lake linatokana na subira ya wazazi wake, ambao kwa muda mrefu walikuwa hawana mtoto wa kiume na Mzee Swalehe akasema ya kwamba mimi nitasubiri na siku alipompata kijana huyo akampa jina la Sihiyana. Hiyo ilikuwa ni mwaka 1926 mwezi



*Sihiyana Swaleh Omari Mhanuka (Mtendamema)*

wa Februari katika kijiji cha Kuuzeni Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani.

Kama ilivyokuwa kwa Mathias Mnyampala (yule mshairi wa Kiswahili) alisoma shule yake

*Endelea uk. 8*

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

## SIKU YA UHURU WA VYOMBO HABARI

**Kila tarehe 3/5/…ya kila mwaka dunia huadhimisha siku ya uhuru wa vyombo vya habari. Siku hii huenda sambamba na kuangalia mchango mkubwa wa vyombo vya habari na wana habari wenyewe kwa ujumla wao. Ni siku muhimu haswa ukizingatia kuwa kila mtu anayo haki ya kimsingi ya kupata habari. Baadhi ya nchi wamekwenda mbali kiasi cha kufikia kuita maswala ya habari kuwa ni muhimili wa nne baada ya ile ya taasisi ya Urais, Bunge na Idara za mahakama.**

**Kila nchi inaweza kuwa na aina fulani ya kuadhimisha na kusherehekea siku hii adhimu kabisa katika haki za binadamu ya kupata habari. Wengi hupenda kuadhimisha siku hii kwa kufanya maswala ya kijamii nk, kwa hapa kwetu siku hii haswa huadhimishwa kwa kufanyika kwa makongamano, semina na hata warsha za aina mbali mbali huku wasomi na wataalam waliobobea katika fani hii ya habari na hata fani nyingine wakitoa mada za aina mbalimbali katika kukumbushana majukumu na misingi ya tasnia hii muhimu katika jamii.**

**Sambamba na maadhimisho hayo, pia siku hii huadhimishwa kwa kuwa na kauli mbiu ya kila mwaka, kauli mbiu hii haswa inategemeana na mambo ya kimsingi yaliyoikumba tasnia katika kipindi cha mwaka mzima. Hapa ikimaanisha matatizo na hata mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya tasnia yenyewe. Mwaka huu hapa kwetu tulikuwa na kauli mbiu inayosema "USALAMA NA MAZINGIRA BORA YA KAZI KWA WAANDISHI"**

**Kauli mbiu hii haikuzuka tu, bali ilitokana na mengi yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka mzima. Kama si hali hiyo ya matatizo na misukosuko waliyokumbana nayo waandishi, bila shaka mwaka huu tungekuwa na kauli mbiu labda isemayo waaandishi wa habari na mabadiliko ya katiba, kwani nchi yetu pia inapita kwenye kipindi kingine kigumu na cha msingi cha uandikishwaji wa katiba mpya. Hakuna ubishi kuwa, wana habari ndio nguzo muhimu sana katika kufanikisha hili. M/Kiti wa tume hiyo ya mabadiliko yakatika aliwahi kusema katika moja ya mikutano yake na wana habari kuwa "wana habari ni nguzo muhimu ya ufanikishaji wa zoezi hili".**

**Usalama wa wanahabri ndio kilio kikubwa kwa mwaka huu, kumekuwa na matukio kadhaa ya kusikitisha kwa wanahabari, ambayo baadhi yao wameumizwa vibaya, wengine hata kupoteza maisha. Matukio kama haya si ya kushangaza sana kwani yamekuwa yakitokea mara kwa mara kwa watu tofauti, lakini kinachoumiza zaidi ni pale ambapo matukio haya yanaponasibishwa kwa namna moja ama nyingine na taaluma hii ya uandishi wa habari. Mengi yatasemwa juu ya matukio haya, lakini mwenye jukumu la kweli la kulinda waandishi na kusema nini haswa kilichojiri ni serikali yenyewe. (kikatiba) Bila shaka baada ya uchunguzi na upelelezi, serikali itatoa tamko na kwa baadhi ya matukio imesha toa.**

**Kwa upande wa wana habari wenyewe, makongamano, matamko, semina nyingi zimetolewa kuhusiana na mada hii, lililo kubwa ni kwa waandishi kuwa makini na kuangalia usalama wao, usalama kwanza mengine baadae. Tasnia hii ya uandishi nayo ina waandishi wengi, vyombo vingi vya habari, uhuru mkubwa hasa wa vyombo vya habari na wanahabari wenyewe, hii ni nzuri mno katika kutekeleza yale majukumu na haki ya msingi ya kupashana habari, jambo la kujiuliza hapa ni je kweli kama waandishi tunalitimiza hilo katika misingi na hadhi yake? Sisi tunapata mashaka kidogo juu ya hili, kwani siku hizi kuna kitu kipya kwenye tasnia ya habari haswa radio FM, kitu kinaitwa "FREE STYLE" ya utangazaji, basi '*ufree*' huo unakwenda mpaka unajiuliza huu nao ni uandishi? Utasikia wakiongea mambo ya kitoto, nje ya maadili ya kiuandishi na hata ya kijamii, mambo katu usiyoweza kuyatamka kadamnasi n.k, wengine hucheka cheka sana bila sababu ya msingi, lakini kubwa zaidi ni pale wanapozungumzia kitu cha kimsingi huku wakionyesha kutokuwa makini, kama vile hawaelewi wanazungumza nini, hili ni tatizo. *Free style* hizi za utangazaji nazo kwa kiasi fulani zinapunguza yale maadili na misingi ya uandishi wa habari, haswa kwenye radio zetu za FM, ukitaka kuona tofauti hiyo kwa kina, fungua hizo FM radio kisha fungua TBC radio, jibu utalipata.**

**Kwa hiyo wakati tukiangalia siku hii muhimu, hatuna budi na sisi wenyewe kama waandishi kujua misingi yetu na majukumu yetu katika jamii, hatuna budi kuwa makini na kazi hii muhimu, kufanya ya kweli bila kuongozwa na vishawishi nk, wema na mahali pake, kama ni kipindi cha michezo, 'cheka' lakini kama ni maswala muhimu ya kijamii basi na umakini hauna budi kuzingatiwa pamoja na kuwepo kwa huo mtindo huru wa utangazaji.**

**Katika mfumo wa maisha tulionao, sote tuna wajibu, hakuna wa kubakia nyuma, tusiwe mbele kulaumu na kunyoosheana vidole, kama waandishi tuna haki za kimsingi za kuitumikia jamii, tufuate misingi ya taaluma yetu na wale wachache wanaotuharibia tuwe makini nao. Tukiweza kutimiza haya vizuri, basi tutakuwa na kila aina ya sababu za kimsingi kabisa za kudai kwa nguvu zote haki na usalama wetu, na bila shaka jamii itakuwa pamoja nasi. Yote yanawezekana iwapo kila mtu atatimza wajibu wake. Mungu Ibariki Tanzania.**

# 'Nuru ya Ahmadiyya' yaangaza Vancouver

*Kutoka uk. 1*

msikiti mmoja mkubwa kwa nini misikiti mingi midogo midogo isijengwe kutokana na fedha hizo hizo. Lakini kama tutazingatia msingi wa haja basi swali kama hilo haliwezi kuzuka na kimsingi tunao mwongozo kutoka kwa Mtukufu Mtume s.a.w juu ya hilo kwamba: *Innamal Aamalu biniyaat:* hakika matendo hulipwa kwa nia.

Vancouver ndio mji mkuu wa British Columbia na hapa ndipo ambapo wanajumuiya wengi wapo, na kwa kuzingatia idadi ya Waahmadiyya waishio hapa kwa hakika huu si msikiti mkubwa sana. Na kisha tuangaliapo msaada na fadhili za Allah zilizo juu yetu na njia mpya zijifunguazo kwa ajili kuufikisha Ujumbe wa Islam Ahmadiyyat kwa hakika ipo haja ya kuwa na sehemu nzuri na zenye nafasi ya kutosha. Tena pia maeneo yetu inabidi yawe mapana na yawe na nafasi sambamba na wahyi alioupata Masihi Aliyeahidiwa mara kadhaa kwamba: ***wasi'i Makanaka*** – panua makazi yako. Ambapo Mwenyezi Mungu Alimuamrisha kupanua makazi yake na kuyafanya yenye nafasi zaidi.

Ufunuo huu hauna maana tu kwamba tuyafanye makazi yetu na maeneo yetu kuwa mapana na yenye nafasi zaidi kwa ajili ya kupokea wageni wanapotutembelea au wakati wa Jalsa tu bali ina maana pia kwamba misikiti yetu iwe na nafasi ya kusaliwa na watu wengi zaidi.

Tena pia katika zama hizi tunazoishi Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameitwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni Ibrahimu wa zama hizi na ilikuwa ni kupitia Hadhrat Ibrahim ambapo Allah Aliamrisha kujengwa upya kwa Kaaba ambayo ni nyumba ya kwanza iliyojengwa kwa ajili ya kusimamisha umoja wake.

Na sawa na bishara za Allah, ni kwa kupitia Masihi Aliyeahidiwa a.s. dunia hii itapata na kwa hakika inapata kumjua Mungu wa Kweli na kwa hakika Uislam utahuishwa tena kupitia Masihi Aliyeahidiwa a.s. Na kwa maana ya kiroho katika zama hizi lengo la kujengwa kwa Kaaba litatimizwa kupitia Masihi Aliyeahidiwa a.s. na dunia siku sio nyingi italishuhudia jambo hili.

Lengo la kujengwa kwa misikiti ni ili watu wapate kukusanyika pamoja kumwabudu Mungu mmoja na kwa maana hii basi tunalo jukumu la kutoa kipaumbele maalum juu ya ujenzi wa miskiti.

Hivyo kama nilivyosema kilicho cha msingi sawa na mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w ni nia nyuma ya kila tendo na hivyo nia zetu na dhamira zetu zinatakiwa siku zote ziwe ni kusimamisha umoja wa Mwenyezi Mungu na kutangaza ujumbe wake ili watu wengi zaidi wapate kukusanyika chini ya bendera ya Umoja wake na sisi wenywe tupate kuleta mapinduzi ya kweli kwenye hali zetu na za vizazi vyetu na kwa kufanya hivyo sisi na vizazi vyetu tupate kuwa wanyenyekevu mbele ya Mungu.

Ni lazima tufanye kila juhudi kuhakikisha kwamba tunasimamisha sala na tuijaze miskiti kwa lengo hilo kiasi kwamba ianze kuonekana midogo kabisa.

Wakati hiyo itakuwa ndio nia yetu, basi hata msikiti ukioneknaa kwa dhahiri ni mkubwa kiasi gani hautokuwa kwa ajili ya kuonesha watu tu bali utakuwa mkubwa kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu, na Inshallah ninashawishika kufikiri kwamba nyote mnaoishi katika eneo hili, ambao mtaujaza msikiti huu, iwapo mtatimiza majukumu yenu kwa nia thabiti, basi mtafanikiwa katika kuueneza ujumbe wa Islam-Ahmadiyya na wakati huo huo mtapa maendeleo ya kiroho na kwa kukiunganisha kizazi chenu na Mungu Mmoja mtakuwa ni chanzo cha kuyakuza maisha yao hapa duniani na katika maisha yajayo.

Hapo pia mtapata radhi za Allah na mtashuhudia fadhili zake kuu zikikumiminikieni kama mvua. Na wakati fadhili za Mwenyezi Mungu zinapoanza kuwashukia watu, zama ambapo nyoyo zinakuwa na dhamira safi ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu tu, hapo basi katika kila mji watu watawezeshwa kujenga misikiti kadhaa.

Hivyo basi sasa nia zenu ziwe hivi kwamba hatutosubiri tena miaka mingine 30 au 40 ndipo tujenge msikiti mwingine lakini tutaendelea kuufanya msikiti huu na mingine pia itayojengwa ionekane midogo kwa ajili uwingi wa watumaiji wake.

Kwa kuijaza misikiti na kwa kutimiza matakwa ya kumwabudu Mwenyezi Mungu na kwa mujibu wa maamrisho yake kwamba tuyafume maisha yetu yawiane na amri zake tutaendelea kuifanya haja ya kuijenga au kuipanua misikiti yetu kuwa njia ya kujipatia zaidi Baraka za Mwenyezi Mungu na tutaifanya hii kuwa njia ya kujipatia fadhili zaidi na zaidi za Mwenyezi Mungu kila siku.

Hivyo ikiwa leo tunaufungua msikiti huu tukiwa na nia hii basi bila shaka tutakuwa tunashika njia ya kujirekebisha kwa kutokujenga msikiti kwa muda mrefu. Na kwa zile sehemu ambazo bado hakuna misikiti, huko pia, kwa ufunguzi wa msikiti huu, fikra zitaelekezwa juu ya kazi hii muhimu na hilo pia litakuwa kama njia ya kujirekebisha kwenu kwa kutokujenga msikiti kwa kipindi kirefu.

Siku zote kumbukeni kama nilivyosema kabla misikiti inayo sehemu yake na umuhimu wake maalum ambao hauwezi kufikiwa na vituo vya sala au kumbi kama vile unavyofikiwa na msikiti.

Ni kweli kwamba kuwepo kwa ukumbi au kituo cha kusalia kunaiwezesha Jumuiya kuwa na sehemu ya kukutania lakini maungano yale ya kiroho na hisia zile ambazo mtu huzipata kupitia msikiti, hizo haziwezi kupatikana bila ya kuwa na msikiti wenyewe hasa. Hii ni sehemu ya maumbile ya mwanadamu. Hivyo mahali popote ambapo ardhi imepatikana, fanyeni mipango ifaayo ili kujenga msikiti badala ya kujenga kumbi tu au vituo vingine vya Jumuiya. Nimeshawahi kupata taarifa ya sehemu moja hapa Canada kwamba wamepata ardhi na kwa fedha walizonazo wameamua tu kujenga ukumbi lakini ninamshukuru Allah kwamba baadae walibadilisha mawazo yao baada ya kuagizwa kwamba waliangalie jambo hilo upya. Mwenyezi Mungu azibariki sehemu zote ambazo zinafikiria kujenga misikiti na wawezeshwe kufanya hivyo.

Ni ukweli ulio dhahiri kwamba kila msikiti mpya ujengwapo njia mpya za mahubiri hufunguka. Mnamo mwezi Machi nilizindua msikiti huko Valencia Uhispania na taarifa zinazonifikia zinaonyesha kwamba hata wasiokuwa Waislamu wameaza kuulizia juu ya Uislamu na Waislamu wasio Waahmadiyya wameanza kusali katika msikiti wetu huo na wanakuja kwa ajili ya kujipatia elimu kuhusu Jamaat. Inshallah kutoka kwa watu hao, wale walioruzukiwa nyoyo njema miongoni mwao watawezeshwa kuuelewa ujumbe wa Ahmadiyya na kujiunga nao.

Miongoni mwa kazi ambazo Mwenyezi Mungu amemuagiza Masihi Aliyeahidiwa a.s. moja ni kwamba Waislamu wafahamishwe juu ya mafundisho ya kweli ya Islam na kwamba wakusanywe chini ya Uislamu ule ambao ulifundishwa na Mtukufu Mtume s.a.w. na kwamba sheria iliyoteremshwa kwake iweze kuhimizwa.

Mwenyezi Mungu Aliyetukuka

*Endelea uk. 3*

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jumuiya, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jumuiya Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

# ‘Nuru ya Ahmadiyya’ yaangaza Vancouver

*Kutoka uk. 2*



*Sehemu ya waaminio wakisikiliza hotuba ya Ijumaa iliyotolewa na Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. ndani ya Masjid Baitur Rahman Vancouver Canada uliofunguliwa hivi karibuni*

Alimuagiza Masihi Aliyeahidiwa a.s. kupitia ufunuo kwamba: Wakusanye Waislamu wote walio juu ya uso wa ardhi kwenye Dini Moja. Akifafanua ufunuo huu Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Amri hii ya kuwakusanya pamoja Waislamu waishio juu ya uso wa ardhi ni agizo maalum kwangu. Kisha akitoa mfano wa Hadhrat Ibrahimu kwamba Mwenyezi Mungu aliuambia moto kuwa baridi na salama kwa ajili ya Ibrahim na hivyo njia za usalama kwa ajili yake zikafunguka, hivyo na amri hii inaonekana kwangu itakuwa ya aina hiyo hiyo (kwamba njia za kuufikisha ujumbe huu kwa Waislamu wote zitafunguka).

Mwenyezi Mungu anapenda kwamba Waislamu wote waishio juu ya ardhi wakusanywe pamoja kwenye dini ya kweli na jambo hilo bila shaka litatokea na wao watakusanywa pamoja ingawaje hiyo haina maana hayatukuwepo makundi kwa asilimia hata kidogo. Bila shaka tofauti zitabakia lakini zitakuwa ni za kiasi hiki kwamba hakutokuwa na hata maana ya kutajwa kwake.

Hivyo sasa njia ya muongozo kwa wote Waislamu na wasio Waislamu ni kupitia kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. pekee. Katika nchi hii na katika mji huu, kuna malaki ya Waislamu waishio hapa na bila shaka msikiti huu utaamsha hisia na kwa ujenzi wa msikiti huu hisia chanya na hata hasi zitasikika kutoka miongoni mwa Waislamu na miongoni mwa wasio Waislamu, lakini hayo yote yatapelekea kupatikana kwa nafasi nyingi za kuutangaza Uislamu wa Kiahmadiyya, nanyi ni lazima mujiandae kwa ajili ya hilo. Hivyo ujenzi wa msikiti huu utaendelea kuyapanua majukumu yenu moja baada ya jingine.

Kwa uwazi kama mnajiandaa kutangaza ujumbe wa Ahmadiyya bila shaka ni lazima mjiandae pia kukuza hali ya tabia zenu njema pamoja na kukuza viwango vyenu vya masuala ya kiimani. Jambo hili ni muhimu na la lazima sana. Iwapo hamtofanya hivyo, basi kwa kukosekana kulandana baina ya maneno yenu na matendo yenu hakuna hata mtu mmoja atakayetaka hata kukukaribieni. Hivyo ujenzi wa misikiti unapelekea kufunguka kwa njia ambazo watu wanaweza kupata baraka za Mwenyezi Mungu ambazo huzidi kuikuza imani ya mwaminio. Na pia kuna Baraka kadhaa za ujumla kwa jamaat yote kupitia ujenzi wa misikiti, kwa kiwango cha kuifanya akili iduwae.

Mwenyezi Mungu Amezungumzia somo la misikiti mahala kadhaa ndani ya Qur’an. Qur’an tukufu inataja heshima ambayo inatakiwa ioneshwe kwa misikiti na pia inataja sifa ambazo wale wanaotaka kuitunza misikiti ni lazima wawe nazo. Aya ya Quran tukufu niliyoisoma mwanzo inazungumzia kuwahusu watumiaji wa misikiti.

Jambo la kwanza lililotajwa ni kuwa wale wanaoifikia misikiti ni lazima wawe wenye kumuamini Mwenyezi Mungu. Lakini kusema tu kwamba tumeamini haitoshi. Imani iliyotajwa hapa inayo kiwango maalum kinachobidi kifikiwe. Mwenyezi Mungu anasema kwamba iwapo mutafikia viwango hivi vya imani basi ni hapo tu ndipo mtakapohesabiwa kuwa wenye imani iliyokamilika vinginevyo imani yenu itahesabiwa kuwa pungufu.

Kwa mfano Mwenyezi Mungu anasema katika Qurani:

Walisema wanaokaa jangwani: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu; maana imani haijaingia mioyoni mwenu; (49:15).

Hivyo Mwenyezi Mungu Akamwambia Mtume Mtukufu s.a.w. kuwa waambie wasiseme wameamini bali waseme wamejiunga tu na Uislamu, lakini kwa sababu mbalimbali bado hamjapata imani ya kweli. Hivyo kutamka shahada na baadae mtu kujitahidi kukuza imani yake na kukuza maungano na mahusiano yake na Mwenyezi Mungu, na kutekeleza ibada zote zilizoamrishwa, na kuwa tayari kutoa aina yoyote ya muhanga kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kujitolea kidhati kutekeleza amri zote za Mwenyezi Mungu, hilo hasa ndilo jambo lenyewe ambalo mtu analotakiwa alifikie baada ya kuukubali Uislamu na hali hiyo ndiyo anayotakiwa awe nayo kila muumini - muumini wa kweli. Hivi ndivyo anavyotakiwa awe kila Ahmadiyya ambaye amemkubali Imam wa zama na hivyo akajiunga na Jamaat yake. Kwa maneno mengine Ahmadiyya anatakiwa aonyeshe dhihirisho la alama hizi za imani katika maisha yake ya kila siku. Mtu azihisi sifa hizi zikiwa ndani yake.

Kuhusiana na hilo Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kwamba waaminio wa kweli ni wale watu ambao matendo yao yanatoa ushahidi wa imani yao ya ndani. Imani inakuwa imenakshiwa kwenye mioyo yao. Na wanalifanya jambo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu kuwa ni la muhimu sana kwao na wanalipa kipaumbele kuliko masuala yote mengine. Na wanashika njia zile zilizo nyembamba na za ndani za taqwa na uchamungu kwa ajili yake tu. Wanazama moja kwa moja kwenye mapenzi yake Mwenyezi Mungu na kila sanamu linalosimama kwenye njia yao kama kikwazo, iwe ni kusinzia kitabia, au udhaifu mwingine wowote au kuanguka, wanajitenga mbali kwa haraka na kitu hicho.

Hivyo hivi ndivyo viwango ambavyo tunatakiwa tuvifikie na tukusudie kuvifikia. Na pale ambapo tutavifikia viwango hivi ni hapo tu tutakapokuwa na haki ya kujiita tuliomuamini Mungu.

Juu ya tafsiri hii ambayo Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameitoa kwamba mtu akanyage njia zile zilizo nyembamba na za ndani za taqwa na uchamungu, hizo ndizo njia mbazo zinamtaka mtu atimize wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu na pia atimize wajibu wake kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu na ahakikishe kwamba kila kiungo na sehemu ya mwili wake inashiriki katika kutimiza amri za Mwenyezi Mungu.

Wakati ambapo mnakizuia kila kiungo na sehemu ya mwili dhidi ya kufanya uovu mnatakiwa pia mhakikishe kwamba mawazo yenu yanakuwa safi dhidi ya uchafu wowote. Iwapo mtafanya hivi, basi katika ibada, katika sala, mawazo yenu yatabaki kumuelekea Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na ni hapo tu ndipo mtakapofanikiwa katika kusimamisha sala.

Iwapo mawazo yenu yote yamezama kwenye masuala ya kidunia na starehe zake tu basi hamuwezi kamwe kumueleka Mungu katika sala zenu. Mtu kama huyo kwa dhahiri anaweza kuonekana akisali lakini mawazo yake yapo mbali yakitangatanga ovyo sehemu nyingine.

Kisha Mwenyezi Mungu amesema wale ambao mawazo yao muda wote yamezama kwenye Mapenzi ya Mwenyezi Mungu ni hao tu ndio waaminio wa kweli.

Mtukufu Mtume s.a.w. ameielezea hii kuwa ni sifa maalum ya mwaminio kwamba kutoka sala moja hadi nyingine moyo wake unabaki ukishikamana na msikiti. Mtu huyo anachokisubiria ni hiki tu kwamba kutoka sala iliyopita, muda wa sala nyingine ufike ili arudi msikitini.

Bila shaka kufanya kazi za kidunia (za kutafuta riziki) pia ni jambo la lazima na muhimu na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameliweka hili wazi kwamba mtu yule asiyetekeleza wajibu na majukumu ya kidunia yaliyo juu yake pia ataulizwa na Mwenyezi Mungu.

Haijalishi ni kzi ya aina gani mtu anafanya, kazi yoyote, iwe biashara, ukulima au chochote kiwacho. Kitu muhimu kinachotakiwa ni hiki kwamba wakati tupo kati kati ya shughuli zetu za kidunia mawazo yetu yote na kwa muda wote yabaki kumkumbuka Mwenyezi Mungu na mtu atakayekuwa anamkumbuka Mwenyezi Mungu muda wote akiwa kwenye shughuli zake basi atajiona kwamba katika shughuli zake hizo anatekeleza pia amri ya Mwenyezi Mungu na hivyo atajaribu kutekeleza wajibu wake na kufanya kazi zake kwa uaminifu na ukweli.

Na mtu huyo atajitahidi asijichukulie faida ya nafasi yoyote isiyo halali kutokana na mazingira ya kazi yake. Basi matendo ya kidunia ya mtu kama huyo nayo pia huhesabiwa kuwa hatua za maendeleo yake ya kiroho au matendo ya kidini kwani mtu huyo muda wote huwa na mawazo ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na mawazo ya ukumbuko wake.

Mifano iliyotukuka ya maisha ya masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. ipo mbele yetu sio kwa ajili ya kufaidi simulizi za maisha yao tu. Lengo lake pia sio kuwa wasifiwe kwa sababu ya matendo yao. Wao hawana haja hata chembe ya sisi kuwasifia au kuelezea maisha yao, Mweneyzi Mungu Ameshawasifia na amewapatia cheti yeye Mwenyewe kwamba Mwenyezi Mungu yuko radhi nao. Basi jambo hili pia mulikubuke kwamba yule ambaye Ameridhiwa na Mwenyezi Mungu hana haja kuwa mtu yeyote amtaje au amsifie.

Bali bila shaka ni kweli kuwa mifano yao inatuhakikishia kwamba iwapo tutakanyaga nyao zao na kufuata mifano ya maisha yao na tutekelza majukumu na kazi zenu za kidunia mkizingatia kwamba lengo lenu ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu pekee basi Mwenyezi Mungu atawawekeni ninyi pia katika wale ambao wanatembea juu ya njia iongozayo kwenye radhi zake.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kuwa iwapo mnataka mfikie viwango vya juu vya imani basi hamna budi mfikie kwanza viwango vya juu vya tabia njema. Na njia ya kupima viwango vya tabia zenu njema ni kuangalia ni kwa kiasi gani mnatimiza haki za viumbe wenzenu. Hivyo kutekeleza sala tu pekee na kisha kwa namna mnayoitaka wenyewe kutimiza wajibu wenu kwa Mwenyezi Mungu hakutoshi kuwahakikishia kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu. Ni jambo la lazima kwa mwaminio kutimiza pia wajibu wake na kutimiza haki za jamii ambayo anaishi ndani yake.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema pia kwamba ni lazima mjiepushe na uvivu na kupoteza muda bure kwani mambo hayo pia humuweka mtu mbali na Mungu. Muda mwingi ukiwauliza wale wanaoona shida kutekeleza sala zao tano za kila siku – na ninawauliza mara nyingi watu kama hao – utagundua wakisema kwamba wanajisikia uzito na hawachukui hadhari itakikanayo. Uvivu humfanya mtu asijali mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kutokuchukua kwake hadhari na kudharau kwake kidogo kidogo lakini kwa uhakika humfanya mtu awe mbali, mbali kabisa na imani na mtu hupoteza hofu juu ya siku ya malipo na hofu ya kutokea kwa siku ambayo atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu na kuhukumiwa.

Hii ndio sababu Mwenyezi Mungu ameitaja sifa ya kuamini maisha yajayo kuwa ni miongoni mwa sifa za wale wanaoiimarisha misikiti na ambao hufika kwa kudumu. Hii ndio sababu tunafundishwa kwamba tutapata malipo ya yale tuyatendayo duniani hapa kwenye maisha yajayo.

Sifa nyingine za wale wanaoiimarisha misikiti ni kusimamisha sala zao mara tano kwa siku pamoja na kujitolea mali zao. Wanatumia mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kupata radhi zake.

Kwa fadhili za Allah Jamaat Ahmadiyya inayo jazba iliyokwenda mbele mno juu ya kujitolea muhanga wa mali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Angalu lipo kundi ambalo linajitolea mali kwa kiwango cha kushangaza. Kwenye ujenzi wa msikiti huu wako wanajumuiya waliojitolea malaki ya dola. Juu ya ujenzi wa misikiti ni kweli kuwa hata wale wasio waahmadiyya hujitolea sana, lakini sifa maalum ya waahmadiyya ni hii kwamba huendelea kwa kudumu kutoa michango yao ya kawaida kutoka mapato yao ya kila siku na kisha haja maalum inapowekwa mbele yao hushiriki. Hii ndio sababu kujitolea kwao kunabeba kiwango cha umuhimu na thamani maalum hasa katika dunia ya leo ya kujali kipato tu na pia zaidi katika siku za leo ambapo kila mahala kuna muanguko wa kiuchumi. Mwenyezi Mungu awabiriki na azibariki mali zao baraka isiyo na mwisho wale wote waliojitolea.

Lakini ninataka mukumbuke jambo hili kwamba kufanya tu wema mmoja hakutoshi kukuwezesheni kufikia viwango vya juu vya taqwa au kuifanya imani yenu kuwa ni iliyokamilkika. Kwa hakika kwa ajili ya mwaminio, mwaminio wa kweli, ni lazima atimize zote: haki za Mwenyezi Mungu na haki za viumbe wa Mwenyezi Mungu.

Sehemu zingine Qurani tukufu inataja sifa nyingi za mwaminio wa kweli na hapa nitazitaja chache kwani ni kwa kuzishika hizo tu ndipo mtu anaweza kusemwa kwamba ameshika njia iliyonyooka sawa na

***Endelea uk. 4***

# 'Nuru ya Ahmadiyya' yaangaza Vancouver

*Kutoka uk. 3*

anayeweza kusemwa kwamba ametimiza haki za msikiti.

Mwenyezi Mungu anasema: ***wal-lazeena aamanoo ashad-do hub-ban lil-lah.***

Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana; (2:166).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema kwamba kilele cha Mapenzi kwa Mwenyezi Mungu ni kumuabudu na hii ndio maana neno *mahabat* hasa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee.

Kisha akasema kuabudu kuna sehemu kuu mbili. Moja ni mtu kumhofu Mungu inavyopasa kuhofiwa. Hofu ya kweli ya Mwenyezi Mungu humfikisha mtu kwenye chemchem ya utakaso na roho yake huyeyuka na kutiririka kumuelekea Mwenyezi Mungu na rangi ya kweli ya kujitupa kwa Mwenyezi Mungu huzalika ndani yake.

Hii ni sehemu moja inayohusiana na hofu ambayo huufanya moyo wa mtu uyayuke na kuanguka kwa sijida mbele ya Mwenyezi Mungu na matokeo yake mtu hujitahidi kutekeleza wajibu wake wa kuabudu na kujitahidi kufikia kuwa mtumishi wa kweli wa Mwenyezi Mungu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Sehemu nyingine wa kuabudu ni kwamba mtu ampende Mwenyezi Mungu kwa jinsi Anavyostahiki kupendwa. Hii ndio maana imesemwa: *wal-lazeena aamanoo ashad-do hub-ban lil-lah:* Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana; (2:166).

Hii inamaanisha kwamba mtu atambue kuwa mapenzi yote ya kidunia ni ya muda mfupi na yenye kuyeyuka na mtu aamue kuwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu ndilo lengo lake kuu. Hizi ndizo haki mbili kuu ambazo Mwenyezi Mungu anazitaka kutoka kwa viumbe.

Hofu na mapenzi ndio mambo mawili ambayo inaonekana kana kwamba haiwezekani kuwa nayo kwa wakati mmoja. Inawezekanaje mtu anayemwogopa mwingine, tena awe na mapenzi juu yake wakati huo huo? Lakini hofu na mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu vina maana na rangi nyingine kabisa. Kwa jinsi kiwango cha mtu kinavyopanda katika kumhofu Mwenyezi Mungu ni kwa kiwango hicho hicho ndivyo yanavyokuwa pia mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu. Na kwa upande mwingine ni hivyo hivyo kwamba kwa jinsi mtu anavyokwenda mbele katika kumpenda Mwenyezi Mungu ndivyo hivyo hivyo inavyoongezeka hofu yake juu ya Mwenyezi Mungu. Na hofu hii inamsawaa kiasi hiki anajizuia kufanya kosa lolote kwa kumafanya achukie sana kufanya maovu na jambo hilo humpandisha daraja na kisha daraja nyingine ya utakaso.

Hii ndio hali ambayo mwamainio wa kweli inambidi aifikie.

Kisha Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaendelea kueleza mapenzi haya ya Mwenyezi Mungu na akasema kwa ajili ya mtu kupata hofu ya Mwenyezi Mungu inambidi ajitupe kwenye maombi na kwa ajili ya kupata mapenzi inambidi ajitupe kwenye ibada ya hija, - lakini hii ni mada nyingine.

Hivyo hii ndio hali ya mwaminio wa kweli, ambayo inambidi aifikie. Ili kwamba hofu ya Mwenyezi Mungu iwe njia ya yeye kupata mapenzi Yake na mtu anapofikia hali au daraja hii hapo tu ndipo anapoweza kuabudu kwa uhalisia wake, anapoweza kuwa mtumishi wa kweli na na ndipo anapoweza kufikia daraja ya kusemwa kuwa ametimiza haki za msikiti ambazo mwamainio anapaswa kuzitimiza. Na hii ndio daraja ambayo Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipenda ifikiwe na kila mmoja aliyemkubali yeye.

Hivyo kwa ujenzi wa msikiti huu tunahitajika kujichunguza zaidi, kujifanyia tathimini sisi wenyewe na kuangalia ni kwa kiwango gani tunatimiza masharti ya kumpenda Mwenyezi Mungu na pia kuangalia ni kwa kiwango gani tunatimiza haki zilizo juu yetu kwa viumbe wengine kwa sababu wajibu wa kuabudu hauwezi kutimizwa bila ya taqwa, (uchamungu) na huo hauwezi kufikiwa bila ya kutimiza amri zote za Mwenyezi Mungu. Allah ametupatia amri nyingi ndani ya Quran Tukufu na mwaminio anatakiwa azitekeleze zote ili kwamba afikie kuwa muumini wa kweli. Kabla nimezieleza chache na ninaomba nitoe ufafanuzi wa jambo moja kwenye aya niliyoisoma.

*Mwenyezi Mungu anasema fa asaa ulaaika anyaqoono minal muhtadeen (9:18).*

Ikimaanisha kwamba hao ndio watu ambao huenda wakafikia lengo la kuumbwa kwao.Hii haikusudiwi kwamba iwapo watafanya amali hizi 'asaa / huenda' wakahesabiwa kuwa miongoni mwa walioongoka.

Hiyo sio maana yake, kwamba iwapo watafanya amali njema kwa ikhlasi huenda wakahesabiwa kuwa wamefikia lengo lao n.k. (kwa maana ya kuwa si jambo la uhakika). Hivyo sivyo kabisa. Wale wote watambuo misemo ya Kiarabu wanajua kwamba neno 'asaa' (huenda) linapotumika kumuhusu Mwenyezi Mungu linamaanisha kuwa jambo hilo ni la uhakika. Na kwa hapa ni kwamba wale wote walio thabiti katika imani yao, na wanatoa zaka na kujitolea mali zao kwa njia zingine, kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu, na hawamuhofu yeyote zaidi ya Mwenyezi Mungu basi hao ndio watu ambao kwa hakika wameongoka mbele ya uoni wa Mwenyezi Mungu na kufika msikitini kwa watu hao na kusimamisha kwo sala na kutekeleza amri zingine zote za Mwenyezi Mungu kutapelekea imani yao na taqwa yao kukua zaidi.

Basi bahati njema ni kwa wale ambao miongoni mwetu wanahesabiwa mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu kuwa wameongoka na wamekuwa wa Mwenyezi Mungu na wanaendelea kuwa karibu zaidi na zaidi na Mwenyezi Mungu.

Sasa wacha pia nitaje majukumu mawili hivi ambayo yamewekwa juu yetu na Mwenyezi Mungu Aliyetukuka katika aya hii: ***Kuntu khaira umatin ukhrijat linaas ta'muruuna bil ma'ruufi watanhauna 'anilmunkar***

Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu, mnaamuru yaliyo mema na mnakataza maovu. (3:111).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu Ametaja sifa ya mwaminio wa kweli kwamba siku zote aamrishe mema na kukataza maovu na kazi hiyo haiwezi kufanyika hadi pale matendo na maneno ya mtu yanapolandana barabara. Iwapo matendo yetu yako tofauti na maneno yetu, basi hotuba zetu haziwezi kuwa na athari hata juu ya watu wetu sembuse kuwa na athari juu ya wengine.

Kwa ujenzi wa msikiti huu kama nilivyosema kabla, njia za kuufikisha ujumbe kwa wengine zitafunguka zaidi, lakini iwapo matendo yetu hayatokuwa kama yanavyotakiwa yawe, kama vile Mwenyezi Mungu alivyoyataja yawe, basi sisi hatutokuwa kamwe umati bora bali pia hatutokuwa miongoni mwa waaminio wa kweli mbele ya Mwenyezi Mungu. Na sala na maombi yetu hayatokuwa na maana yoyote na hata kujitolea kwetu mali hakutokubaliwa na Mwenyezi Mungu na yale madai yetu kwamba tunayo hofu ya Mwenyezi Mungu nyoyoni mwetu yatakuwa ni ya uongo.

Basi ni wajibu wetu wa mwanzo kabisa kuhakikisha kwamba tunayafuma maisha yetu ili yaende sambamba na amri za Mwenyezi Mungu.

Agizo lingine la Mwenyezi Mungu ni hili kwamba: ***waquulu linaasi Husnaa:*** ... na semeni na watu kwa wema (2:84).

Utimizaji wa kwanza wa amri hii unatakiwa uwe miongoni mwetu wenyewe hasa wale waliobeba majukumu ya kiofisi wanatakiwa walijali zaidi jambo hili. Kabla hatujatoka nje kuwaita wengine, lazima kwanza tuijaze misikiti yetu na wataabadi ambao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wanatimiza haki za Mwenyezi Mungu kwa kumuabudu ipasavyo.

Wakati mwingine ninapokea malalamiko kwamba baadhi ya maofisa wanazo tabia au wako wanaojidhani wenyewe kuwa wamefikia viwango vya juu vya utawa na hivyo wanaongea na watu kwa namna ambayo inawaachia maumivu ya kifikra na hivyo kuwatupa nje kabisa ya Jamaat. Watu kama hao badala ya kuiimarisha misikiti na kuifanya ifikiwe na watu wanasababisha ikimbiwe.

Hivyo ili kufikia kuwa watu bora ni lazima kwanza tujisahihishe sisi wenyewe.

Kisha kama ilivyotokezea mara nyingi kupitia ujenzi wa misikiti, njia mpya za kuufikisha ujumbe wa Islam Ahmadiyya hufunguka ndivyo hivyo pia itakavyotokezea hapa. Inshallah. Hivyo watu watakapofika kuuona msikiti, au miongoni mwa marafiki zenu watakapofika kukutembeleeni, ni lazima mkuze na muendeleze athari hii kwamba siku zote Waahmadiyya wanatenda wema kwa wengine.

Hiyo ndiyo athari na hisia ambazo tunalazimika tuzikuze na tuzibakishe duniani kote kuhusiana na Mwahmadiyya. Hili ni fundisho la Islam kwamba badala ya kujipendelea tu sisi wenyewe tuwapendelee kwanza wengine. Na hili sio liwe jambo la kufikirika tu bali liwe la kutekelezwa kivitendo, na sasa kwa kufunguliwa msikiti huu watu wanatakiwa walione jambo hilo zaidi na zaidi.

Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, anafungua njia mbalimbali za kuufikisha ujumbe wa Islam Ahmadiyya. Wakati mwingine tunapata kuwasiliana na kukutana na watu ambao ingekuwa vigumu kuwasiliana au kukutana nao ambayo hiyo nayo si matunda ya juhudi yetu sisi wenyewe binafsi; na Inshallah mtaona hapa pia kwamba mawasiliano na mahusiano ya aina hiyo yatapatikana. Basi kwa matendo yenu mzishinde nyoyo juu ya mahusiano hayo kwa kuzifanya ziupende Uislam na mafundisho yake.

Hivyo kama nilivyosema utendaji baina yenu na watu wengine uwe kwa ajili ya kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na mapenzi hayo yakuwe, na nyote mtowe umuhimu maalum kwa jambo hili kwani hili ni jambo la lazima kwetu kwa ajili ya kuutangaza ujumbe wetu na kuiimarisha Jumuiya yetu na pia ni jambo la muhimu kwa kila mmoja wetu ikiwa anataka kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Ajaalie kwamba kwa kujengwa kwa msikiti huu Jumuiya iimarike zaidi kwa ndani na iwe ni sababu ya kutekelezwa zaidi kwa amri za Mwenyezi Mungu kama hii ya watu kuijaza misikiti na nyoyo za wale watakaofika hapa muda wote zibaki kushikamana na msikiti kwa njia ile ile ambayo Mtukufu Mtume s.a.w. alipenda kila muumini aifikie. Msikiti huu uwe ni njia ya kuvutia fadhili na baraka za Mwenyezi Mungu na kila yule atakayeutembelea msikiti huu apate sehemu ya baraka hizo na njia za kuusambaza ujumbe wa Islam Ahmadiyya zifunguliwe zaidi kama matunda ya kujengwa kwa msikiti huu.

Juu ya gharama na ukubwa wa ujenzi wa msikiti huu Huzur alisema huenda usiwe wa umuhimu sana kwa wakazi wa hapo lakini kwa walio nje wanaweza kuvutiwa nao:

Tangazo la ujenzi wa msikiti huo lilitolewa mwala 1997 na Hadhrat Khalifatul Masih IV r.h. na yeye mwenyewe akaupa jina wakati huo kuwa ni Masjid Baitur Rahman. Umesimama kwenye eneo la ekari nne kasorobo ukiwamba futi za mraba 33,419. Ni wa ghorofa mbili. Una kuba lenye urefu wa futi 47 na mnara wenye urefu wa futi 76 kwenda juu. Kumbi mbili kubwa za kusalia wanawake na wanaume na zikichanganywa zinafanya eneo la futi za mraba 6,800 ambazo zinaweza kuruhusu watu 1,132 kusali ndani yake.

Kuna nafasi ya kupaki magari kama 140 na kumbi zingine ndogo ndogo zinazoweza kubeba hadi watu 1,050 na hivyo kama zote zitumike kwa ajili ya sala msikiti huo unaweza kusaliwa na watu wapatao 2000. Pia kuna maktaba, ukumbi maalum kwa ajili ya Tabligh, jiko, sehemu ya huduma za mazishi, vyumba vinne vya madarasa, vyumba kadhaa vya ofisi, ukumbi wa mkutano, makazi ya mbashiri, na nyumba ya wageni. Msikiti umepambwa kwa nakshi nzuri ya maandishi. Gharama za ujenzi zinafikia Dola za Canada milioni 8.5, Mwenyezi Mungu Aubariki msikiti huu kwa ajili yenu kwa kila njia.

Mwishoni ninapenda kusoma nukuu fupi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliyosema:

Uzuri wa kweli wa msikiti haumo katika uimari na uzuri wa jengo lake bali uzuri hasa umo kwa wale wanaosali sala zao humo kwa unyenyekevu wa hali ya juu. Bila ya watu kama hao misikiti ni kama iliyowachwa mitupu. Msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w. ulikuwa mdogo na paa lake liliezekwa kwa makuti ya mtende kiasi kwamba wakati wa mvua ulikuwa ukivujisha. Lakini mng'ao wa mazingira ya msikiti umo kwa wanaofanya ibada humo. Katika zama za Mtukufu Mutme s.a.w., watu wenye mawazo ya kidunia waliwahi kujenga msikiti ambao ukabomolewa kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Msikiti huo ukapewa jina Masjid Zarar na kisha ukabomolewa. Hivyo amri ya kujengwa kwa misikiti imo kwenye msingi kwamba ni lazima ijengwe kwa makusudio ya uchamungu na utawa.

Hivyo hili ndilo jambo ambalo kila Ahmadiyya ni lazima alizingatie.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameendelea kusema:

Jumuiya ni lazima iwe na misikiti yake ambamo Imam Mwanajumuiya aongoze sala humo na ambaye awaase na kuwaongoza watu na hasa wanajumuiya wakusanyike humo kwa ajili ya kutekeleza sala za jamaa kwenye msikiti huo.

Kuna baraka nyingi ndani ya Jumuiya wakati tutakuwa kitu kimoja na kuna mkanganyiko mtupu iwapo tutafarakana. Na hizi ni zama ambazo umoja na udugu unatakiwa uhimizwe zaidi na vijambo vidogo vidogo vinavyoweza kuleta utengeno visitiliwe sana maanani.

Mwenyezi Mungu Atusaidie kuyafuma maisha yetu yaende sambamba na maagizo haya. Ameen,

# Kisa cha Nabii Issa (a.s.) Kusema Uchangani

*Kutoka uk. 1*

ewe Mariyam bila shaka umeleta jambo jipya. Ewe dada wa Haruni baba yako hakuwa mtu mwovu wala mama yako hakuwa asherati. Akamwashiria kwake (Isa) wakasema tutazungumzaje na mtoto mdogo aliye mbelekoni"?

Wengi wanadhani kuwa aya hizi zinaeleza tukio Iililochukua nafasi mara tu baada ya kuzaliwa kwa Nabii Isa (as). Na kwa hiyo wanaamini kwamba Mariyam alimleta mtoto huyo kwa jamaa zake mara baada ya kujifungua akiwa amempakata. Ndipo wakamtuhumu kupata mtoto nje ya ndoa, jambo ambalo ni chukizo kubwa katika mafundisho ya Torati lililostahili adhabu ya kifo. Lakini ikiwa dhana hii ni sahihi, basi jambo hili linakanganya zaidi. Kwanza badala ya Mariyam mwenyewe kukabili tuhuma hizo kwa utetezi wake binafsi, anaonekana kumtupia mzigo huo mtoto mchanga ambaye hakuwa na uhusika wowote juu ya tuhuma hizo. Pili katika majibu anayoyatoa mtoto huyo hagusii lolote kuhusu tuhuma hizo, bali anaonekana kuhubiri tu juu ya unabii wake! La kushangaza zaidi hata baada ya tuhuma hizo kukosa utetezi wa kufaa kutoka kwa Mariyam na mwanae, bade aliachwa aendelee kuishi badala ya kuhukumiwa adhabu ya kupigwa mawe hadi kufa kwa mujibu wa sheria. Bila shaka maswali haya yanatufanya tutafakari zaidi juu ya hekima na maudhui hasa yaliyomo katika aya hizi.

Kwa vyovyote vile dhana hii ilianza kuzalika kutokana na maneno 'WA AATAT QAUMAHAATAHMILHU' (na akamleta kwa watu wake akiwa amempakata), wakalifasiri neno TAHMILHU kuwa ni kupakata au kubeba mbelekoni. Bila shaka imesahaulika ya kuwa neno hili la lugha ya Kiarabu humaanisha kubeba tu. Iwe kubeba mimba, kubeba mtu au mzigo mgongoni au mabegani na hata kumbeba mtu juu ya kipando chochote.

Maana hii ya kumbeba mtu juu ya kipando pia inatajwa katika kamusi maarufu ya Lisanul Arab (tazama chini ya neno HAML) vilevile kamusi ya Tajul-Arus Jz.7, uk.28.

Kimsingi neno HAML limetumika katika aya mbalimbali za Qur'an likimaanisha kubeba kwa namna yoyote na haliashirii tu kupakata. Neno hili limetumika juu ya wanyama wanaobeba mizigo yetu (16:8), limetumika kumhusu mwanadamu aliyebeba amana itokayo kwa Mola wake (33:73) limetumika vilevile kwa maana ya Mwenyezi Mungu kuwalinda na kuwaongoza watu katika bara na bahari (17:71). Maana hiyo iliyotajwa katika kamusi tulizozirejea, yaani kumpandisha mtu juu ya mnyama kama vile ngamia, farasi, punda n.k imetumika pia katika Qur'an tukufu (9:92) pale kinapotajwa kisa cha baadhi ya masahaba waliotaka kushiriki vita Fulani wakakosa wanyama wa kuwatumia na hivyo kumwendea Mtume (saw) iii awapatie wanyama wa vipando. Mtume (saw) alikosa wanyama wa kuwapatia na hivyo wakakubaliwa udhuru wa kutoshiriki vita.

Katika aya zote tulizozirejea hakuna mahala lilipotumika kwa maana ya kupakata. Na kwa hivi kutokana na ufafanuzi huu ni wazi kwamba neno hili hata lilipotumika katika aya ile inayomhusu Nabii Isa (as) haiashrii kuwa alikuwa amepakatwa. Tunaona hapa kwamba neno HAML lilipotumika kuhusu mwanadamu kumbeba mwanadamu mwenziwe ni pale tu Iilipomhusu Mtume (saw) na masahaba zake (9:92). Kwa vyovyote iwavyo maana hii ndiyo inayosadifu mno tukirejea kwenye tukio la Mariyam kumbeba nabii Isa (as).

Basi kwa hali hii tukio linalozungumzwa katika aya tunazozijadili haliwezi kuwa ni la kupakatwa kwa Nabii Isa katika 'baby show' mara tu baada ya kuzaliwa. Kwa hakika aya hizi zitakuwa zinarejea tukio moja ambapo Nabii Isa (as) wakati ameshakuwa Nabii mwenye wafuasi alipandishwa juu ya punda akiwa amefuatana na mama yake pamoja na baadhi ya wanawake wanaomtumikia na kuingia Yerusalemu (Marko 11:7-11), Mathayo 27:55-56). Maana hii ndiyo yenye mantiki inayoeleweka, kwa maana inaingia sana akilini hapa ikisemwa kuwa ndio wakati Mariyamu alikuwa akimleta mwanawe kwa watu wake akiwa amembeba juu ya punda.

Wengi wanaoamini kuwa aya hizi zinazungumzia tukio la wakati wa uchanga wa Nabii Isa (as) yumkini wamekanganywa na kutokana na kuulinganisha mfuatano wa maelezo na mfuatano wa matukio. Maana Qur'an Tukufu mara tu baada ya kueleza tukio la kuzaliwa kwa Nabii Isa katika aya ya (19:24 - 26) ghafla katika aya inayofuata inaeleza tukio hili la kuletwa kwake akiwa amebebwa. Ni kweli ya kwamba kutokana na mfuatano wa m aelezo ulivyo, yeyote aisomaye Qur'an Tukufu kwa kulinganisha na kitabu cha simulizi za kale lazima aishie katika kushika dhana hii kwamba Isa (as) alizungumza katika umri wa uchanga. Lakini imesahaulika kwamba (Qur'an) imewalaumu mno wale wanaoifananisha Kurnai na visa vya watu wa kale (83:13-14).

Ifahamike ya kuwa Qur'an Tukufu imeandikwa kwa mfumo wenye hekima ya ajabu, kwa hivi kuelewa maudhui na mpangilio wake pia kunahitaji hekima ya hali ya juu. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Anasema 'Bila shaka tumewafululizia kauli'.

Basi katika kutafakari hekima na maudhui yaliyo katika aya tunazozijadili ni lazima tutafakari juu ya aina ya mfululizo uliowekwa katika aya zinazozitangulia. Bila shaka kuna hekima kubwa kwa Qur'an Tukufu kutanguliza kwanza uzaliwa wa Nabii Yahya kila anapotaka kueleza uzaliwa wa Nabii Isa (as). Na hivi ndivyo ilivyofanyika katika aya hii.

Kwa hivi, kama mtu anataka kuelewa hali ilivyokuwa katika maisha ya Nabii Isa (as) mtu hana budi kuelewa hali ilivyokuwa katika maisha ya Nabii Yahya (as). Kuna sababu nyingi zilizopelekea hali hii, nazo ni kwamba Manabii hawa yumkini waliishi wakati mmoja, walitumwa kwa taifa moja, misukosuko na masaibu yaliyowapata yanafanana kwa kiasi Fulani. Hali kadhalika, Iicha ya kuwa Manabii hawa walikuwa ndugu wa damu, lakini pia namna ya kuzaliwa kwao wote wawili ilikuwa ni ya utata mno. Nabii Yahya alizaliwa na wazazi wawili mama aliye tasa rn baba aliyeishiwa nguvu za kiume.

Nabii Isa (as) amezaliwa na mwanamke bikira asiyepata kujuana na mwanamume.

Basi ni kama hivi ndivyo ulivyo mpangilio wa maelezo yao. Hadithi zao zimepangiliwa kwa kufanana na kufuatana katika aya za Qur'an Tukufu. Unaweza kuona kwamba katika aya ya (19:8-10) bishara ya kuzaliwa kwa Nabii Yahya inatolewa, katika aya ya (19:11) baba wa Nabii Yahya Hadhrat Zakariya anapewa maagizo ya kufunga saumu, aya ya (19:12) Hadhrat Zakariya anawatokea watu mihrabuni ghafla katika aya ya (19:13) Nabii Yahya anapewa utume kwa kuambiwa ashike kitabu kwa nguvu. Haielezwi hata habari ya mama yake alivyoshika mimba, alivyomzaa na hata maisha yake ya utoto na makuzi yake hayatajwi. Kwa usomaji wa kikasuku mtu anaweza kudai kuwa Nabii huyu alipewa Unabii akiwa bado angali mbegu katika mgongo wa baba yake.

Naam! Wapo baadhi ya wafasiri waliokanganywa hasa na hili pia, hasa kutokana na aya ya 13 inavyomalizia "Na tukampa hekima akiwa bado mdogo", wakaamini kuwa Yahya alipewa ufunuo wa kinabii akiwa mtoto mchanga.

Kwa kila hali maneno 'kamata kitabu kwa nguvu' yanaashiria kuwa ni ufunuo aliopewa Nabii Yahya akiwa tayari yu mtu mzima anayefaa kuwa Nabii wa Mwenyezi Mungu.

Qur'an Tukufu hapa haikuwa ikitoa simulizi za maisha ya Nabii Yahya, bali ilikuwa ikirejea matukio muhimu tu katika maisha yake.

Ni mfululizo wa aina hii hii ndio uliotumiwa katika fungu Iililofuata linalozungumzia maisha ya Nabii Isa (as). Kwani katika fungu hila pia kuanzia aya ya 19:20 -22 bishara ya kuzaliwa kwa Nabii Isa (as) inatolewa, katika aya ya 23 Mariyamu anashika ujauzito, aya ya 24 - 26 inataja kuzaliwa kwa Nabii Isa (as), katika aya ya 27 Mariyamu anapewa maagizo ya kufunga yanayofanana nay ale aliyopewa Zakariya katiak aya (19:10).

Hatimaye katika aya 28 - 33 Nabii Isa anapelekwa mbele ya watu na kuanza kuzungumza maneno ya kinabii.

Kwa hakika, kama ilivyokuwa katika fungu lililotangulia kumhusu Yahya (as), ndivyo ilivyo hapa. Aya hizi zinakumbusha juu ya tukio lililotokea wakati Nabii Isa (as) ameshapevuka na kupewa ufunuo wa kinabii na wala hakuwa king'ele aliyepakatwa.

Isingewezekana kwa Hadhrat Isa kutoa madai aliyotoa katika majibu yake kama asingekuwa ni mtu mzima kwani aliposema kuwa "Amenifanya kuwa Nabii" (19:31) yaonyesha kuwa alishakuwa bwana Fulani, kwani Qur'an Tukufu inatangaza kuwa Mwenyezi Mungu Hakuwatuma Manabii kabla isipokuwa RIJAAL (wanaume) aliowafunulia (21 :7) neno RAJUL katika lugha ya kiarabu humaanisha mwanamume mtu mzima. Katika ayah ii pia Hadhrat Isa (as) anadai kuwa amelazimishwa kusali na kutoa zaka muda wote wa uhai wake. Amri hii haingii akilini kwamba Mwenyezi Mungu aitoe juu ya kichanga kilichopakatwa. Kwa mujibu wa sheria za Islam sala huwa ni lazima kwa mtu aliyefikia baleghe yake. Na hali kadhalika mtoa zaka, siyo tu anatakiwa awe mtu mzima, bali pia awe mwenye kipato cha ziada. Mtoto mchanga ambaye hana kipato chochote zaidi ya maziwa ya mama yake hana wajibu wala uwezo wa kutoa zaka. Juu ya hayo aya inayofuatia inataja amri ya kumsaidia mama yake kwa wema. Mtoto mchanga ambaye hawezi hata kujisaidia mwenyewe atatekelezaje amri ya kumsaidia mama yake?

Bila shaka kuwapo kwa amri hizi juu ya Nabii Isa (as) kunawezekana tu pale alipokuwa mtu mzima mwenye nguvu na kipato. Maneno yanayokaririwa hapa kuwa yaliyosemwa na Isa (as) bila shaka aliyasema akiwa mtu aliyekwishapevuka na kupewa unabii. Ala kuli hali fungu la aya tunazozijadili, halielezei matukio ya uchangani mwa Hadhrat Isa, isipokuwa ni tukio lililochukua nafasi ilihali Nabii huyu amekwishatimiza umri wa miaka 40 au angalau kama ilivyokisiwa na Luka mwandishi wa Injili miaka 30. (Luka 3:23) ambapo ndipo Yesu alipoanza kazi ya kuhubiri utume aliopewa na Mungu.

Kwa mujibu wa maelezo ya Injili ni kwamba mahubiri ya Yesu katika Uyahudi yalidumu kwa mwaka mmoja. Katika muda huo Yesu aliingia katika masinagogi na kujadiliana na wakuu wa dini wa Kiyahudi, Mafarisayo, Masudukayo na Waandishi. Hawakuwa tayari kumwelewa, walipokea ujumbe wake kwa chuki na ubishi mkubwa. Hili lilimdhoofisha na kumkatisha tamaa Nabii wa Mungu. Katika kuonyesha kuchukizwa kwake na tabia yao, Yesu alipata kuwaita watu hao kwa majina mabaya kama vile wanafiki, vipofu, nyoka, wana wa ibilisi na hata kizazi cha zinaa (yaani wanaharamu) tazama Mathayo 23:16 -23), Mathayo 10:38, Yohana 8:44). Kutokana na walichokiita kuvunjiwa heshima, Masheikh wa Kiyahudi waliazimia kuufutilia mbali ujumbe wake, wakijipanga kuzuia silsila yake isiendelee, walifika mbali zaidi na kuazimia hata kuyakatisha maisha yake kwa hila.

Inavyoelekea ni kwamba katika zama hizo baraza la wazee (Makuhani) wa Kiyahudi lilikuwa na mamlaka ya kumshitaki Myahudi yeyote, lakin; halikuwa na mamlaka ya kutoa hukumu hadi pale hukumu hiyo itakapothibitishwa na Pilato. Kanuni hii ilitiliwa nguvu zaidi endapo shitaka lilihusu adhabu kubwa kama vile adhabu ya kifo (Yoh.18:31). Kwa hali hii Makuhani waliazimia kumfitini Nabii Isa kwa kumzushia kesi ambayo waliamini ingeweza kumletea adhabu ya kifo. Ndipo wakamzushia tuhuma ya kwamba anadai Ufalme na kwamba anawashawishi watu wasilipe kodi kwa Kaisari (Tazama Yohana 19:12 na Luka 23:2). Bila shaka tuhuma hizi zililenga kumzushia kesi ya uhaini ambayo aghalabu adhabu yake ilikuwa ni kifo.

Lakini kwa mujibu wa sheria za utawala wa Kirumi, adhabu yoyote isingeweza kutolewa mpaka kwanza mtuhumiwa ahojiwe. Ikiwa atakana shitaka lake, mashahidi wasiopungua wawili walihitajika kuthibitisha tuhuma hizo. Huu pia ulikuwa ndio utaratibu wa uendashaji wa mashitaka katika kanuni za Kiisraeli za Talmud. Ndiyo maana Nabii Isa anaonekana wakati Fulani akihojiwa na Kuhani Mkuu kuhusu mashitaka hayo (Yohana 18:19-21). Katika majibu yake, Nabii Isa anaonekana kuwapa changamoto nzito Washitaki wake kwa kuwataka wawaulize mashahidi juu ya madai yake kwa kuwa yeye hakuwa na ajenda yoyote ya siri.

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Bustani ya Washairi

Huwezi kulazimisha beti kwa jambo lisilo rohoni. Haiwi na haitakuwa. Ukiona shairi limetoka safi basi maizi ya kwamba jambo hilo limemgusa mtunzi. Jambo hilo limemuathiri. Binadamu hana njia ila kukimbilia kwa Mola wake ili apate hifadhi. IIi apate ulinzi. IIi apate utulivu. Ndivyo anavyofanya Mmatumbi Asilia wa kutoka Duthumi Morogoro Bi. Muhaimina Hamidu. Anajitupa mbele ya kizingiti cha Mola wake akiomba sitara.

1. Bismillahi naanza, kwa jinale lotukuka
Nisifa zake Muweza, ni yeye Mkamilika
Hakuna anayeweza, isipokuwa Rabuka
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

2. Subhaana Mola wangu, zipokee dua zangu
Nisamehe dhambi zangu, natubu makosa yangu
Utakase moyo wangu, nakuomba Mola wangu
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

3. Nalia mimi nalia, mwenzenu nalia sana
Kwa Mola sishi kulia, natubu kwake Rabana
Naomba kwa kutulia, nijalie Subhanna
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

4. Naomba kwa kutulia, nijalie Maulana
Upate kunijalia, mema yalojaa sana
Na Kwako nakimbilia, Unilinde E Rabbana
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

5. Umeniumba dhaifu, kwa ubavu ulopinda
Ee Mola Mtukufu, kazi ya Mola mtenda
Unijalie Latifu, mazuri nipate tenda
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

6. Mimi ni mama wa wana, wawili wape salama
Waishi kwa kufaana, nakuomba Ee Karima
Uwaruzuku Rabbana, uwape na taaluma
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

7. Bushirati, Nasrati, E Mola wape akiri
Wasiende na wakati, uwape na kufikiri
Wawe ndani ya Jamaat, wafate zako amri
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

8. Uwaongoze Latifu, wana kwenye msafala
Uwape na ubunifu, wasifanye ya papala
Elimu ni mara dufu, waende na Kampala
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

9. Ee Rabbana Mtukufu, uniepushe na shari
Nakuomba Ee Latifu, na dhana nazo hatari
Nitadumu mara dufu, kuepuka nazo shari
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

10. Naomba kwa jina lako, na sifa zilizo njema
Msaada toka kwako, nina kuomba Karima
Unilinde mja wako, niishi kwa usalama
Nisitiri Mola wangu, zipokee dua zangu

11. Morogoro ya kusini, Wilaya ya vijijini
Duthumi langu tawini, na waaga kwaherini
Sote tumo safarini, tumuombe Rahmani
Kukosea binadamu, kufunzana ni wajibu

**Bi. Muhaymina Hamidu (Mmatumbi Asilia)**
**Duthumi - Morogoro**

## HITILAFU YAKE NINI?

Afrika tuko njia panda. Tuna mila na desturi zetu. Hayo tumeyaacha. Tumeyatelekeza. Kwa pupa tumechukua yasiyo yetu. Hayo ya wengine tumeyavamia. Wala hatupendezi. Nguo ya kuazima. Tufanye nini anauliza Z. Ally Mussa (Mtu wa kuliwa) wa Dar es salaam.

1. Toka mwenye usingizi, mzalendo usilale
Limelia dudumizi, jimbi nalo liwikile
Amka unibarizi, haya na ya siku zile
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

2. Yale tuliyoyaponda, yasiote tena pale
Tukayang'oa kwa inda, na kujichuna vidole
Na haya tuliopanda, hebu unielezile
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

3. Ya kale yalitushinda, hayapendezi umbole
Ndipo hatuku yapenda, haya nayo vilevile
Hayagusiki kwa chanda, matawiye miba tele
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

4. Yale mbaya harufuye, na haya tuyapandile
Yaukakasi tamuye, heri na njaa ulale
Hebu ni fafanuliye, yepi mema tuyaole
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

5. Hitilafu yake nini, kati ya haya na yale?
Wa kwamba ipo ni nani, hirimu au mvyele?
Haya yetu ubaini, nayo yalopita kale
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

6. Jaribu kujituliza, utame kitamatile
Ufanye kuyachunguza, ewe mja polepole
Kisha utanieleza, mimi na wewe tulole
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

7. Kalamu naweka chini, hapa ndipo nikomile
Kama ipo niauni, falau kwa mizingile
Mimi kamwe siioni, ni namna ile ile
Kati ya haya na yale, hitilafu yake nini?

***Shaabani Gonga bingwa wa kufutu hoja. Analo jibu mutribu. Jibu kuntu. Moja ya shairi bora linaloeleza utamaduni wa mtu mweusi.***

1. Limepigwa gurumizi, tumeitwa wasanifu
Tutoke mwausingizi, tuzitoe hitilafu
Ya kale na siku hizi, yepi yenye ukakafu?
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima.

2. Tumetupa beedani, tukazidharau afu
Vikaasiwa vipini, kadhalika vishaufu
Ni vipuri vya zamani, vilileta unadhifu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

3. Tukautupa mkadi, uturi wawatukufu
Sasa twasema hamadi, bagubani yatukifu
Tuliubetua udi, hivi sasa umedhoofu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

4. Tukaisukuma hina, tena kwa kuikashifu
Leo na miti hakuna, imelala safusafu
Ni nini kitacho fana, kitacho faa halafu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

5. Iliketwa asumini, tukamba mbaya harufu
Ilitumiwa mijini, na mabinati shufufu
Leo bora baniani, anaonwa mnadhifu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

6. Zilivaliwa debwani, na vitambi vitakafu
Mavazi mpaka chini, tuendapo nefunefu
Yakalaniwa nchini, tukamba vazi hafifu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

7. Sasa yako mataiti, na nywele za watu wafu
Yale ya kale hayati, walakini ashirafu
Kwa mimi hamnipati, haya ya leo kusifu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

8. Ingawa kuna vitundu, mwenye majumba marefu
Havishi vipindupindu, na watu kututakifu
Na umetadi utundu, kutupokonya minofu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima.

9. Imetandawaa dhara, kila mtu ana hofu
Vyetu vina tekwa nyara, twalia watu ulufu
Mgawaji wa ngawira, hugawa kwa upungufu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

10. Gubi tumegubikizwa, yalivyo yametukifu
Kusema tunakatazwa, twaamriwa kusifu
Kwa kweli tumetatizwa, hayakupwi maji mafu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

11. Nakomelezakomango,twalazwamwenyeminyefu
Na hayeshi masimango, twasimangiwa madafu
Tena haishi mipango, mamia kwa maelfu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

12. Nitamatile kitumi, tumacho bali madufu
Mtu gani atuhami, tumpe utakatifu
Nimemaliza usemi, haya kwa wingi machafu
Yale yana uraufu, kwa hadhi na kwa heshima

Lipyoto kachafua mto. Wa kule wanadhani ni hawa ndiyo wamechafua mto. Lakini haikuwa hivyo. Zamani wakichinja wale na hawa wanakula. Wanakaribishana wakati wa siku kuu inaanguka pilau. Mjomba Mwislamu, Shangazi Mkristo. Pameingia nini? Saa ya Msikitini inasema saa tatu na ile ya Kanisani inasema saa saba. Wakati majira ni yale yale? Sihiyana Salehe Mandevu (Mtendamema) anawaita Washairi warekebishe saa hizi

1. Saa zetu hivi sasa, majira hazilingani
Si za kwenye Makanisa, wala za Misikitini
Zimeachana kabisa, sijui sababu gani
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

2. Saa hazendi sawia, washairi karibuni
Nyingine hutangulia, nyingine zenda mwishoni
Nyingine hung'ang'ania, kurabu hazigusani
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

3. Hasa zile kubwa sana, zile za viwambazani
Hazitaki kulingana, na hizi za mikononi
Hii husema mchana, ile husema jioni
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

4. Saa zikituongoza, hata iwe ya dukani
Huna haja kuuliza, uionapo makini
Sasa zinatupoteza, sijui tutanye nini?
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

5. Sasa hazikidhi haja, zimeondoka thamani
Hazina majira moja, faida hatuioni
Mimi nasema vioja, vijana kusanyikeni
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

6. Kuna saa nyingi sana, nyingine za mifukoni
Husema kwa mnong'ono, wa karibu huioni
Ila hukupa mfano, unapokwenda kazini
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

7. Saa zikituandaa, kwa mema ya maishani
Hukataza yasofaa magomvi na tafurani
Hutwepusha na balaa, akhera na duniani
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

8. Saa huwa kama kinga, hata ndogo za mezani
llipo hupata mwanga, kiza hubana pembeni
Ni fyagio la ujinga, mijini na vijijini
Washairi kuna nini, saa hazendi sawia?

## ULIMWENGU WETU

1. Jina la Mola ndo kambi, nami ninakimbilia,
Ili anipe ulumbi, wa vina kupangilia,
Kati ya tungo tutumbi, yangu isije ingia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

2. Kuna wetu ulimwengu, tuliojichagulia,
Una ladha kama kungu, ndugu zangu nawambia,
Kwetu hakuna ukungu, giza tumelikimbia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

3. Tumerefushwa mikono, mgongo twajisugua,
Tunajilia vinono, ni supu kwa vitumbua,
Tunabarikiwa mno, kila tunapopumua,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

4. Tunairamba asali, hamu inapotujia,
Hatuitafuti mbali, ndani tumejijazia,
Hatutumii nauli, ladha kuisafiria,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

5. Tunakula wali nazi, kwa viungo miamia,
Tunakula kwa mchuzi, vizuri unonukia,
Tunashushia kwa ndizi, tunda tunalotumia
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

6. Twakuta ndani liwazo, moyo unapoumia,
Yakitujaa mawazo, faraja hukimbilia,
Vitokeapo vikwazo, Mola Anatukingia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

7. Ulimwengu wetu pepo, si kufuru naapia,
Wanaishi kama popo, humu wasioingia,
Nami nashika kiapo, humuhumu nitafia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

8. Ulimwengu wa maraha, si peke niloingia,
Hata bwana Mafutaha, huku amekimbilia,
Atembea kwa madaha, Kalindima akimbia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

9. Bwana Makame wa Tanga, tunda kashajivunia,
Mkongwe Jamili Mwanga, mbona ameshaingia,
Mtekateka katinga, mama kanichukulia
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

10. Abdalla wa Msese, kakayo hajakwambia,
Mboga twaunga mawese, kwa nyanya na mabamia,
Fanya bidii unase, vitamu uje jilia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

11. Raisi Mwakitalima, huku kumemnogea,
Kila apatapo nema, heka hujiongezea,
Waone kina Ndatama, wanavyojinenepea,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

12. Hakika nusu ya dini, sisi tumejitwalia,
Kama nanyi mwatamani, basi ifateni njia,
Mje ingia kundini, pepo kuikaribia,
Huu ulimwengu wetu, una ladha kemkem.

**Lutufu A. Mbanga (Utu busara)**
**S.L.P 1 MOROGORO - 0655133337**
**lutufumbanga@gmail.com**

# "Mwelewe Maulvi Nuruddin"

# Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

*Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq*

**Kutoka toleo lililopita**

**MANDHARI YA MWISHO**

"Nashuhudia kwamba hamna mwabudiwa isipokuwa Mungu, na ninashuhudia kwamba Muhammad ni Mtumishi Wake na Mjumbe Wake, (mara mbili).

"Leo, katika Jumiya Ahmadiyya, natubu kwa dhambi zote juu ya mkono wa Mahmud, na kwa kujaaliwa na Mungu nitajibidiisha kuepukana na dhambi zote katika siku zijazo; sitamshirikisha Mungu na chochote, nitatanguliza dini juu ya mambo ya kidunia, nitajaribu kutekeleza maamrisho yote ya Islam, na nitakutii katika mema yote utakayoniamuru.

Nitamwamini Mtume Mtukufu kuwa *Khatamun Nabiyyin;* nitaamini madai yote ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.; na nitatia bidii kuzagaza Islam.

"Namwomba Mungu, Mola wangu, msamaha kwa dhambi zote na ninatubu kwake (mara tatu).

Mola wangu, nimejidhulumu nafsi yangu. Nakiri dhambi zangu, na ninakuomba Unisamehe dhambi zangu, kwani hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe."

Alipokwisha kuchukua baiati, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akafanya dua ndefu ya kimya, na kila mmoja akaungana naye, na akamalizia kwa hotuba fupi.

Hivyo wanajumuiya waliokuwa wanahangaika na kuachwa katika ukiwa wakaunganika mara nyingine katika udugu wa kiroho. Nyoyo zote zikatulia, na roho zote zikapata raha. Kila mmoja akapata msukumo mwema wa ndani kabisa. Ukunjufu na utulivu ukaenea.

Hadhrat Khalifatul Masihi II r.a. akasalisha sala ya jeneza ya Hadhrat Khalifatul Masihi I r.a. Halaiki ya watu, Waahmadiya, wasiokuwa Waahmadiyya, Mabaniani, Masingasinga, Wakristo, wanaume kwa wanawake na watoto, wakajumuika wote kumsifu yule ambaye ukarimu wake ulikuwa kwa wote bila ubaguzi, ambaye moyo wake ukafurika mapenzi na huruma kwa wote. Kabla halijachwa jua mwili wake ukazikwa upande wa magharibi wa rafiki yake mpendwa, Masihi Aliyeahidiwa a.s., ambaye kwa ajili yake aliwaacha wote.

Mola, uifanye mvua ya rehema Yako inyeshee kaburini pake;

Umwingize peponi kwa rehema Yako.

Magazeti ya sehemu zote za nchi yakataja sifa bora za mkarimu huyu wa ubinadamu. Hapa twaweza kueleza moja au mawili tu.

*Zamindar* likaandika:

"Miongoni mwa habari zilizopokelewa kwa simu ya maandishi leo, kuna habari itakayowahuzunisha Waislamu, hususan Waahamadiyya, ya kifo kilichotokea Machi 13, baada ya maradhi yaliyoendelea kwa wiki kadha, cha Maulawii Hakim Nuruddin Sahib, aliyekuwa Sheikh mtaalamu na mwanachuoni aliyeelimika. Sisi ni wa Mungu na Kwake tutarejea.

Maulawii Hakim Nuruddin alijulikana baina ya wafuasi wake kama Khalifatul Masihi na alikuwa mwenye kushika uongozi baada ya Mirza Ghulam Ahmad. Kifo chake ni msiba mkubwa kwa Waahmadiyya watakaouhisi kwa muda mrefu. Mbali na hitilafu za kiitikadi, dhati na vipawa vya Maulana Hakim Nuruddin vilikuwa vya hali ya juu sana hata kwamba Waislamu wote watahuzunika kwa kufariki kwake. Yasemekana kwamba inahitajika karne nzima kudhihirika mtu mwenye akili halisi ya kuvuta macho. Leo tunaomboleza kifo cha mtaalamu mashuhuri wa dini. Tunawapa pole marafiki zetu Waahmadiyya ambao wamepata uchungu wa msiba huu mkubwa. Twaomba Mungu, Mwingi wa ukarimu Amwingize Maulawii Hakim Nuruddin katika rehema Yake na kuwajaalia wafuasi wake na watu wa familia yake subira."

Mhariri wa *Curzon Gazette* akaandika:

"Si tu kwamba tulimjua marehemu Maulawii Hakim Nuruddin, tulijuana sana kikamilifu tulipokuwa huko Jammu kwa miaka mingi. Tukaonana kila jioni. Alikuwa na moyo mwema na mkarimu. Alikuwa mcheshi, mchangamfu. Alikuwa tambo la mtu, mzuri wa sura, mwenye rangi nzuri na ndevu nyingi. Alisimamia shule za serikali na hospitali kwa bidii na uaminifu. Alipata mshahara mkubwa ambao sehemu yake kubwa aliitoa kwa ukarimu wake kwa posho na matumizi ya wanafunzi waliohitaji msaada. Katika maisha yake yote aliwaruzuku mamia ya wanafunzi wenye hali ndogo. Sheikh Abdullah, kijana wa Kikashmiri aliyekuwa Brahmin (Baniani) akasilimu kwa mafunzo yake. Akamsaidia na akamtolea gharama yote ya masomo ya shule na ya elimu ya juu mpaka akawa wakili (mwanasheria) na akaimarisha kazi yake ya uwakili katika Ali



*Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.*

Garh. Sheikh Abdullah alipenda sana kuwaelimisha wanawake na akaanza kutoa jarida *Khatun* (Mwanamke) kutoka Ali Garh.

Basi, Hakim Nuruddin alikuwa mfano hai wa ukarimu wa kweli. Alikuwa na jazba mbili, kufanyiza ustawi wa wanafunzi wenye hali ndogo na kukusanya vitabu vinavyopatikana kwa nadra. Mapato yake makubwa yalikuwa yote kwa miradi hii miwili. Alikuwa mnyenyekevu sana na mwenye staha. Alitimiza wajibu wake wote kwa unyofu. Waliofanya kazi chini yake walipendezwa naye, hawakuwa na manung'uniko. Alikuwa Sheikh mtaalamu na mwanachoni mkubwa; alikuwa bingwa wa Kiarabu. Katika saa zake za faragha alitoa darasa la *Bukhari* na *Muslim*. Alikuwa na utambuzi mwingi wa dini."

Maulana Abul Kalam Azad, aliyekuwa mwenyewe mwanachuoni mashuhuri na mwanasiasa, halafu akawa Mwenyekiti wa All-India Congress, na waziri wa Elimu katika Serikali ya India, akaandika katika *Al-Balagh*, chini ya maelezo mafupi ya habari:

"Buriani, Nuruddin – Nasikitika kwamba mimi ni wa mwisho kutoa rambirambi juu ya Imam wa Jumuiya Ahmadiyya kutuacha mkono, aliyekuwa mchunguzi hodari wa kweli za daima, Hakim Maulawii Nuruddin. Mtu aliyejikusanyia ujuzi mpana sana pamoja na hazina ya mifano ya kiamali ya utakaso na wema wa kweli hayuko tena baina yetu. Utaalamu katika yote yale yaliyoihusu dini na ujuzi mkubwa wa kweli zote, ukichanganywa na elimu pana iliyoenea kila aina ya vitabu kuanzia maandiko ya dini hadi hadihti bora za kubuniwa, vikanyanyua dhamira ya Nuruddin hadi pale ambapo ikaweza kufikiria na kupenya katika siri ya maono ya binadamu. Ndiyo sababu mshtuo hafifu wa maneno yake machache lakini yenye maana sana ukafumba midomo ya wapinzani wake wenye ufasaha wa kuvutia. Dhati yake nzima ilikuwa mchanganyiko wa utawala wa maono ya kidini na ujuzi. Busara yake iliyoenea ulimwengu mzima ilikuwa wavu wa kisumaku wa hekima. Uchunguzi wake wa kifilosofia ukichanganyika na unyofu kamili ukamtobolea siri za mbinguni. Imani yake timilifu katika hekima ya Mungu ikamtilia moyoni mwake fikara zake zote.

"Sehemu ya mwisho ya maisha yake ilitolewa wakfu kwa Jumuiya Ahmadiyya; siku zake, mchana na usiku, zilitumika katika bidii za kuchosha kwa kupata miradi ya kiroho ya Jumuiya yake. Kujitolea kwake kwa uaminifu na utii halisi alioonyesha kwa mfunzi wake wa kiroho bila shaka yoyote hakuna kifani chake isipokuwa baina ya Waislamu wa zamani. Kusema nabii Isa a.s. alikufa kifo cha ajali, aliyefikiriwa na watu wote kwamba anaishi mbinguni na kiwiliwili chake, na kuchukua Mahdi na Masihi kuwa mtu mmoja tu, ilikuwa ni ujumbe mchungu kwa Masheikh wa Kiislamu wa Bara Hindi, na gharika ya upinzani ambao itikadi hiyo mpya ilisababisha ulikuwa kama radi ya kuteketeza; lakini ukali wa dhoruba hii haukuuathiri uimara wa imani ya Nuruddin. Akasimama imara kama mlima mzito usiotikisika ukiyakabili mawingu yapitayo kasi sana na ngurumo ya mshindo. Uthabiti wake halisi haukuvumilia kwamba aachilie mbali mto wa mawe ambao juu yake roho yake iliyosumbuka na iliyokwenda safari ya kuvumbua habari ikapata raha mustarehe mpaka pumzi yake ya mwisho. Ingawaje siafikiani na baadhi ya itikadi za Jumuiya Ahmadiyya, hata hivyo naangalia sana kwa kushangaa mng'ao wa kiroho ambaomwakowakeumeyeyusha maono yangu yaliyogandamana yakawa machozi yatiririkayo ya mapenzi.

Mheshimiwa Nuruddin sasa amefichikana kwa macho yetu, lakini nyayo zake zinadumu kutambulikana waziwazi juu ya uso wa ulimwengu na zasaidia kutuongoza kwenye jumba la uthabiti. Rehema na huruma ya Mungu imwage marashi ya ambari juu ya vumbi lake."

Hilo ni kumbukumbu fupi la kazi nyingi sana bora za aina mbalimbali ambazo mtu mashuhuri Hafidh Alhaji Hakim Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a. alitenda. Uchache wa nafasi umekuwa kizingiti nisiweze kutoa maelezo marefu. Lakini jiha moja ya huduma yake kubwa ya Uahmadiyya, Uislamu na ubinadamu yahitaji kutiliwa mkazo. Qur'an Tukufu ilitangaza ya kwamba katika zama za mwisho watu wa Kitabu watashirikiana pamoja dhidi ya Islam na kutafuta njia ya kuiangamiza, lakini Mungu Atavunjilia mbali njama zao na Ataishindisha Islam juu ya dini zote (9:30-33). Ushindi huu ulitakiwa kupatikana kwa njia ya Masihi Aliyeahidiwa, si kwa upanga bali kwa kutumia silaha za kiroho. Masihi Aliyeahidiwa akadhihiri, na chini ya maagizo ya Mungu akakusanya ghala ya silaha zile, na kuonyesha namna zitakavyotumika kuzishinda nyoyo za binadamu kwa huduma ya Islam. Akaeleza kwamba ametumwa kwa kuongoza kazi ya kuishindisha Islam na kutoa silaha ambazo kwa kuzitumia hizo Islam itahuika kwa njia ya Jumuiya iliyoanzishwa naye, chini ya uongozi wa *Makhalifa* zake wa kiroho. Akasema, amekwisha panda mbegu itakayochipua ikawa mti wenye matawi yatakayoenea, na kwamba yeyote hataweza kuzuia ukuaji wake. Baada ya kutimiza kazi yake aliyoagizwa na Mungu kutekeleza akaaga mnamo 26 Mei 1908. Msiba huu ulikuwa pigo kubwa mno kwa wanajumuiya ambao walishikwa na butwaa wasielewe wapi kwa kuelekea.

Mungu Akawaimarisha na kwa huruma na rehema Yake Akawaunganisha pamoja chini ya uongozi wa Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. akiwa Khalifatul Masihi. Kulikuwa hamna hata sauti moja isiyokubali. Lakini ole, muda si muda, haraka zaidi mno, minong'ono, si ya kukaidi kwa wazi, bali manung'uniko wa ndani yakaanza kuibuka na kusikika. Baadhi ya wanajumuiya maarufu wakaanza kufikiria demokrasia, Katiba na Mabunge. Walakini, ni ajabu kabisa kwamba wakaipendelea *Sadr Anjuman Ahmadiyya,* ambamo walijikuta kuwa wengi, kama uwanja wao wa kukusanyika, wakisahau, au pengine kwa sababu, hiyo ni chama kinachojifanyiza upya, hakikufanyiwa uchaguzi wala siyo cha kidemokrasia, ilhali *Khalifa* alikuwa wa hao wenyewe, na pia alikubaliwa na wanajumuiya wote. Lakini jiha hii ilikuwa ya kijuujuu tu. Walichopuuzilia mbali kabisa ni kwamba *Ukhalifa* ni daraja la kiroho lililoahidiwa msaada wa Mungu waziwazi kwa kukazania (24:56). Ushindi wa Islam ulikuwa upatikane kwa njia za kiroho chini ya maagizo ya *Makhalifa* walioongozwa na Mungu. Hivyo, ubishi ukazuka. Je, Jumuiya ilikuwa iongozwe na kuelekezwa na kiongozi wa kiroho mwenye madaraka ya mwisho aliyewekwa na kuongozwa na Mungu, ama isimamiwe na kutawaliwa na Chama kilichosajiliwa kinachojifanyiza upya? Kama

***Endelea uk. 8***

# ‘Mtenda Mema’ Kwa Mola Katangulia

*Kutoka uk. 1*

kwa kusikiliza kutoka dirishani, kwani hakuwa mwanafunzi rasmi. Elimu hiyo ndogo aliyoipata ilimsaidia kujenga mapenzi yake ya kusoma. Ndiyo hiyo pia iliyompa fursa ya kusoma magazeti ambayo yaliongeza mapenzi yake kwa ushairi. Magazeti hayo ni pamoja na *Mambo Leo, Mapenzi ya Mungu, Baraza, Mwanafunzi, Kiongozi* na *Baragumu.*

Sihiyana Swaleh Mandevu Mtendamema amepita katika maisha ambayo yamemsaidia kuielewa vilivyo dunia. Kuelewa tamu na chungu ya maisha. Mashairi yake yanatokana na uhalisia wa yale aliyokutana nayo yale yaliyomgusa. Ndiyo maana mashairi yake yana mguso wa ajabu. Ukisoma shairi lake unamaizi kuwa Mtunzi huyo anaelewa vilivyo anachokizungumzia. Kwa mfano shairi lake “Ubaya hauna kwao, Tani boy amezidi” ni shahiri linalopendwa na wale waliokuwa watu wazima kwenye miaka ya hamsini (50). Wengi wao wanalikumbuka kwa ghaibu shairi hilo. Sababu kubwa ni kwamba hivyo sio visa au porojo, hayo ni mambo aliyoyaona kwa macho yake. Wakati akitafuta kazi alifanya kazi ya utingo na hadi akawa dereva. Hivyo aliweza kuviona visa vya utingo ambavyo vinaendelea mpaka hivi leo. Mambo mengine ingawaje hayakumgusa yeye mwenyewe, bali yaliwagusa wale walio karibu naye na hivyo kumpa ukaribu wa matukio hayo. Shairi lake “Mapenzi hayana dawa” linapendwa ajabu. Kwa sababu linagusa ukweli wa maisha.

Mama mmoja wa Mombasa alitiririkwa na machozi alipolisoma shairi hilo na akawa anadhani ya kwamba Mtendamema alikuwa akimsema yeye. Alipokwisha tulia mama huyo kwenye miaka ya 60 alimtumia Shilingi tano (5/=) zikiwa ni hongera kwa shairi lake hilo. Na ikumbukwe katika miaka hiyo shilingi tano hazikuwa ndogo.

Mashairi yake mengni yanagusa siasa. Ipo sababu. Mara baada ya kuacha kuendesha mabasi ya abiria yaliyokuwa yanatoka Dar es salaam kwenda Kisarawe, Mtendamema alimiliki na kuendesha Taxi. Hiyo ilikuwa ni mwaka 1954. Kituo chake kilikuwa karibu na mahali kilipozaliwa chama cha TANU ambapo sasa ni mtaa wa Lumumba. Mwalimu Nyerere wakati huo anafundisha Pugu. Waendesha Taxi wengi walikuwa wanamkwepa John Rupia, kwani walipokodi Taxi aliomba afuweni ili kumchukua Mwalimu Nyerere Pugu, wakati huo chama kilikuwa hakina fedha. Siku moja John Rupia alimwambia Sihiyana awapeleke yeye na Mwalimu Pugu na wakati wanakwenda Pugu akamwambia ‘Mtani wangu huyu Bwana atakuwa maarufu na anapigania heshima ya mtu mweusi’. Toka siku hiyo Bwana Sihiyana akawa na kazi hiyo ya kumleta Mwalimu kwenye mikutano ya siasa na kumrudisha Pugu. Sihiyana pia alikuwa ni mmoja wa viongozi wa mwanzo wa ‘TANU Youth League’ Bwana Sihiyana aliendelea kuwa mwanachama wa mstari wa mbele wa TANU hadi ilipozaliwa CCM, yeye aliendelea kukitumikia chama na alikuwa miongoni mwa Wazee wa CCM wa jiji la Dar es salaam.

Washairi kwa kutambua umuhimu wake katika ushairi walimchagua kuwa Mwenyekiti wa UKUTA Taifa. Katika wadhifa wake huo alihudhuria mikutano mingi iliyokuwa ikifanyika sehemu mbalimbali za nchi. Kwa hakika ni yeye tu aliyeendelea kupeperusha bendera ya UKUTA na Ofisi hiyo iliyo katika jumba la ANATOGLO kama yeye hayupo basi utakuta Ofisi imefungwa.

Bwana Sihiyana aliheshimu utamaduni wa kabila lake la Kizaramo, alikusanya hadithi nyingi na Methali za Kizaramo akiwa na shabaha ya kuzichapisha. Anayo pia mashairi mengi ambayo ameyatunga katika lugha ya Kizaramo. Aliwahi kunipatia muswada wa methali za Kizaramo ambao unafaa kuchapishwa.

Mtendamema alithamini sana utamaduni wa watu weusi. Alisikitishwa sana na wale wanaobeza utamaduni wetu. Kwa vitendo alifanya utafiti wa mila na desturi za Kizaramo, lakini kila siku aliumia. Kwa nini sisi hatuna Alphabeti zetu. Utafiti wake ulimfikisha katika kutengeneza herufi za Kiafrika. Utafiti huu aliupeleka chuo kikuu cha Dar es salaam mpaka sasa hakuna kilichosemwa na chuo hicho juu ya ugunduzi huo. Pengine Vyuo vyetu havimuheshimu mtu mpaka awe na Shahada ya Uzamivu. Mtendamema aliwahi kumuonesha kazi hiyo aliyekuwa Waziri wa Mila na utamaduni Sheikh Kaluta Amri Abedi. Mtenda mema alilalamika kwamba watu walionesha kubeza na kutoijali kazi hiyo. Sheikh Kaluta alimueleza maneno ambayo hata siku moja Mtendamema hakuyasahau.

Alimwambia; ‘Wote waliofanya makubwa hawakupata shangwe mwanzoni, mvumilivu hula mbivu’. Mtenda mema hakukata tamaa mpaka siku zake za mwisho alikuwa akiniuliza kuwa wapi tunaweza kupeleka kazi yake kwa ajili ya uchunguzi zaidi.’

Sihiyana Swalehe Mandevu Mtendamema ameacha mashahiri mengi ambayo tuna wajibu wa kuwarithisha wajukuu wetu. Mashahiri yake ni hazina kubwa. Tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa mistari hii ya johari inawafikia wale wote wanaothamini na kuenzi Kiswahili.

Katika mazungumzo yetu daima alipenda tukumbuke muda mchache tulio nao hapa duniani. Chochote chema tunachotakiwa kukitenda tukitende kwa haraka. Kwani hakuna aliye na madaraka na kesho isipokuwa Allah.

Kifo ni jambo ambalo halikwepeki na ni lazima litatokea. Mara kwa mara tulikuwa tukizungumza juu ya safari hiyo ya mwisho na alipenda sana kunukuu ubeti wa Shaabani Robert usemao;

Siku ya Mauti kuja, mtu hana kimbilio.
Kuja budi itakuja, kama si kesho ni leo
Kila mtu humfuja, bila ya mapendeleo
Habaki mtu mmoja, katika safari hio

Nao ubeti wa Hamisi Amani Hamisi Nyamaume ulipeleka mbali mawazo ya Sihiyana Swalehe Mandevu, ule usemao;

Kufa sisi ni lazima, mauti yametubidi
Kufa kumeanza zama, na hako alokaidi
Wamekufa waazama, na Mtume Muhammadi

Ukurasa tumefunga, unohusu zama zile
Kwa kutawafu nyakanga, mtunzi wa beti tele
Tunamuombea mwanga, apate pepo milele
Mti wetu kuanguka, wapi tupate kivuli?

Sihiyana kwa kutunga, Mtendamema taile
Beti alizifinyanga, za hekima na miyale
Ili tuepuke janga, lenye fujo na kelele
Mti wetu kuanguka, wapi tupate kivuli?

Mambo ya kuvungavunga, ya chembechembe za ndwele
Kwake aliona tanga, na misiba vilevile
Dawamu hakucharanga, maneno yaso simile
Mti wetu kuanguka, wapi tupate kivuli?

Baidi alijitenga, na yaletayo upele
Mithili kama kuringa, kujiona mteule
Hayo yote alipinga, kwa hoja na kwa upole
Mti wetu kuanguka, wapi tupate kivuli?

Kinara mleta mwanga, wa mstari wa mbele
Ukuta aliujenga, kulinda yetu ya kale
Ili wasije tobanga, walo twachia wavele
Mti wetu kuanguka, wapi tupate kivuli?

Kaditamati wahenga, koleo livunjikile
Tulie hadi kutonga, tupate kama wa vile
Yarabi mwenye kupanga, nasi hili tupangile
Mti wetu kuanguka, wapi tupate kivuli?

# Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

*Kutoka uk. 7*

Jumuiya iwe ilivyotajwa nyuma, hapo hiyo haitakuwa Jumuiya ya kiroho na itapotewa na ahadi za Mungu na Dhamana Zake zilizotolewa katika sura 24:56. Swala hilo lililowekwa mbele ya yule shujaa aliyeutetea *Ukhalifa*, Hadhrat Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a. Hakuliepa wala hakulipiga chenga, wala hakuacha hata inchi moja ya ardhi mbele ya tambio na vitisho vya dhahiri na vya siri. Akasimama imara kama mwamba na mawimbi ya manug’uniko na ukaidi yakampigapiga vikali na yakarudi nyuma yakiwa hoi katika bumbuazi kama povu la mshindo mkubwa. Alimtegemea Mungu kikamilifu; akajua kwamba msimamo wake ulikuwa wa haki machoni mwa Mungu. Theluthi mbili za karne zilizopita tangu atuache mkono zimethibitisha ukweli wake machoni mwa binadamu pia.

Kama juu ya swala la daraja na madaraka ya *Khalifa*, Hadhrat Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a., angelilegea hata kama kidogo mno kwa kushurutishwa mfululizo na wale waliojidhania kushika uongozi katika Jumuiya, mti uliopandwa na Masihi Aliyeahidiwa ungelipata kunyauka haraka haraka, kama kwa hakika inavyoshuhudika katika maanguko ya kusikitisha ya kundi la wenye kukaidi na chama chao. Ahadi ya Mungu kuhusu ushindi wa Islam katika zama za mwisho ingelibaki bila kutimia, na jambo hilo lingetilia shaka ukweli wenyewe wa Islam. Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. alikuwa chombo cha Mungu kwa kudumisha na kuimarisha desturi ya *Ukhalifa* ambao kwa njia ya huo ushindi wa Islam ulitakiwa kutangazwa na kuletwa. Namna chombo hicho kilivyofanya kazi vizuri na barabara yaweza kufahamika kutoka katika kurasa za kitabu hiki, na natija za jinsi ya kufanya kazi yake yaweza kushuhudiwa kutokana na ustawi ulioupata mti wa Uahmadiyya. Mzizi wake upo imara na matawi yake yamefikia mbinguni. Huleta matunda yake mapya mapya nyakati zote kwa amri ya Mola (14:25-26). Kinyume chake mti wa wakaidi umeng’olewa ardhini wala hauna uimara (14:27). Ulezi wa Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. ukahakikisha kwamba mbegu iliyopandwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. haina budi kumea na kuimarika, kisha kunenepa na kusimama imara juu ya shina lake na kuwafurahisha wapandaji; ili makafiri wapate kukasirikia hiyo (48:30).

Hiyo ilikuwa kazi ambayo hekima ya Mungu ilimkabidhi Nuruddin r.a.; akaitekeleza kazi hiyo kikamilifu kabisa.

Mungu na Amjalie, kwa rehema Yake na huruma Yake, daraja la juu kabisa katika Pepo za radhi Yake kuwa makazi Yake. Amin.



*Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. - Mtunzi wa kitabu hiki*

## Mwisho

***Kitabu hiki kinapatikana kwenye matawi yote ya Jumuiya nchini na pia kweye tovuti ya Jamaat Ahmadiyya: www.alislam.org***

# Ni nani Mlezi wa Kiswahili?

**Na Al-Ustadh Khamisi Wamwera - Dar es Salaam**

Alhamdulillahi, sifa zote njema zinamhusu Subhana Wata'ala, Mola wa ulimwengu. Kwa hakika miongoni mwa mambo muhimu ambayo mwanadamu yanaweza kumletea maendeleo m akubwa ni Lugha. Lugha ni chombo azizi sana. Kuijuwa lugha vizuri ni elimu, utaalamu na ubingwa. Lugha yetu ya Kiswahili ni ya asili na ya kale. sijuwi kama yupo mtu anaweza kujitokeza kusema lugha hii si ya Watanzania!

Mwanzoni pale, Kiswahili kilizungumzwa janibu za Pwani tu mwa nchi hii. Mikindani kule Lindi, Mzizima Dar es salaam, Bagamoyo, Tanga, Zanzibar, Lamu na Mombasa. Bali sasa Kiswahili kinazungumzwa mikowa yote ya Tanzania. Ni sawa nikisema sasa hivi ni lugha ya Taifa.

Kwa muono wangu, kupanuka kwa lugha ya Kiswahili kumechangiwa na vitu vingi. Nakumbuka vizuri sana mnamo miaka ya 60, Serikali ya awamu ya kwanza ilifanya juhudi ya makusudi kabisa ya kukuza nguvu ya lugha yetu hii. Ilipanuwa uwigo wake kwa kuithamini na kuitilia maanani. Kwa namna hii, Serikali na wananchi wenyewe waliunda vyombo mbalimbali kushughulikia lugha ya Kiswahili. Bali taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, pale chuo kikuu mlimani Dar es salaam, baraza la Taifa la Kiswahili Zanzibar, Bakita, Ukuta na kadhalika.

Naweza kusema vyombo hivyo pale mwanzo vilifanya kazi khasa ya madhumuini ya ya kuanzishwa kwake ambapo hivi leo vinaonesha kuchoka. Pale mwanzoni vyombo hivyo viliweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kupanuwa uwanja wa lugha ya Kiswahili. Zamani Kiswahili kilizungumzwa Tanzania, Kenya na Uganda tu, hali ya sasa si hivyo. Leo lugha ya Kiswahili inazungumzwa Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo hadi visiwa vya Comoro. Si hivyo tu, bali vituo mbalimbali vya radio vinakitumia Kiswahili katika baadhi ya vipindi vyao. Kwa m fano, kituo cha utangazaji cha Muslim Televisheni Ahmadiyya (M.T.A) kilichopo jijini London Uingereza kinarusha baadhi ya matangazo yake kwa Kiswahili. Vituo vingine vinavyorusha matangazo kwa Kiswahili ni BBC London, Sauti ya Amerika, Ujerumani na Japan. Na vituo mbalimbali vya radio vinatumia Kiswahili katika baadhi ya vipindi vyao.

Naam, hata kwenye baadhi ya mikutano ya nchi huru za Afrika, Kiswahili kimepiga hodi. Kimetumika Kiswahili kama moja ya Lugha rasmi katika mikutano yao. Hili limethibitika pale Rais mstaafu wa Msumbiji Mheshimiwa Joaquim Chisano alipozungumza kwa mara ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili kule Ethiopia miaka kadhaa iliyopita. Hapana shaka, hii ni njia mojawapo ya kukienzi Kiswahili.



*Shaaban Robert - Mtunzi maarufu wa vitabu na mashairi ya Kiswahili*

Tarehe 12 Marchi 2013, kwa msaada wa Allah nilijaaliwa kuhudhuria sherehe ya uzinduzi wa kitabu cha historia ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi kilichoandikwa na Hayati Mathias Eugen Mnyampala Wamachichimi (Penda chako) wa Dodoma pamoja na kitabu cha historia ya Hayati Mathias Mnyampala kilichoandikwa na Daktari Matei Roy. Sherehe hii ilitayarishwa na watoto wa wazee hao wawili mjini Dar es salaam.

Sherehe hii ilifanyika kwenye ukumbi wa Karimjee kuanzia saa nne asubuhi hadi saa nane mchana na mgeni rasmi alikuwa Mzee Kingunge Ngumbare Mwiru. Binafsi nilinufaika kuona watu wengi mashuhuri wenye hamu na shauku kubwa wanaotaka Kiswahili kikuzwe na kiheshimike wamefika pale. Mmoja Bwana Amiri Abdallah Sudi Andanenga (Sauti ya kiza).

Watoaji khutuba karibu wote waliwasifu manju hawa wawili, Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi (Shahid) na Bwana Mathias Mnyampala kwa juhudi zao walizoonesha katika kukikuza Kiswahili kwa kukisema na kwa maandiko yao mbalimbali.

Nikubaliane na wakhutubu hao kwayo. Kwani ni kweli kabisa kwamba malenga hao wawili wamefanya kazi kubwa kwa muda mfupi. Bwana Mnyampala ameishi miaka 52, naye Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi (Shahid) alikuwa wa miaka 40 tu. Ukitazama kwa makini, mambo waliyoyafanya khususa katika kuhami na kukikuza Kiswahili ni kubwa kuliko miaka yao waliyoishi manyakanga hawa. Ukitazama kazi zao unaweza kudhani wakati wanaondoka katika dunia hii walikuwa wa umri wa miaka 80 hivi au mia moja.

Unaweza kushangaa, kwa mfano Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi (Shahid) alisoma muda gani hapa nchini na n je ya Tanzania! Angalia mpaka anafariki, alikuwa na watoto 7. Ninahisi hapa somo lipo nawaachia wataalamu.

Mtu wa namna hii, aliyefanya juhudi ya kila aina kuwaongoza wenzie kwenye njia ya Mwenyezi Mungu, kamwe hawezi kuwa shujaa aliyesahauliwa. Huyu aliyetowa neno "BUNGE" na kukubaliwa, "IKULU", likaafikiwa na akafanya kila juhudi Kiswahili kisemwe kwenye Bunge hilo, nasema aslani hasahauliki. Ni mtu juhula anayebeza almasi hii ya Afrika. Bali naona nchi itakuwa na makosa tena makosa makubwa kama haitathamini kazi adhimu ya Mzungupule huyu katika kukienzi na kukikuza Kiswahili.

Niipongeze Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya kwa kumpa heshima anayostahili Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi (Shahid). Kwa jicho lako la chongo wewe hukuliona hili, lakini historia imeona ukweli na kuunukuu. Ni nani aliyeandika kitabu cha *Sheria ya kutunga mashairi na diwani ya Amri*? Ni nani aliyeandika kitabu cha *Uongofu wa Tafsiri ya Qur'an Tukufu* kwa Kiswahili faswaha kama kile? Wewe hukujaaliwa kumsikia kwenye radio Tanzania akizungumza na kutetea umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili badala ya Kingereza pamwe alikijuwa vyema Kiingereza. Ni yeye na mabingwa wenzie aliyekuwa anabonga kwenye kipindi cha mbinu za Kiswahili. Shujaa wa namna hii asahauliwe! Hapana, hasahauliwi abadani. Gazeti la Mapenzi ya Mungu mara kwa mara huwa linatowa khabari na shughuli muhimu alizofanya Maulana Sheikh. Tafadhali Mudir endelea kutuletea uhondo. Sheikh atakumbukwa daima kwa sababu za kazi zake njema za kuhudumia watu.

Hapa napenda kuiomba Serikali kwamba ifanye uamuzi wa kijasiri na kweli wa lugha ya Kiswahili kuwa ndiyo lugha ya Serikali, lugha ya Taifa. Ijaribu, bali ifanye shughuli zake zote kwa Kiswahili. Ijapokuwa kauli ya kusema hivyo ipo, lakini kwa kweli ipo kinadharia wala haionekani katika matekelezo yake.

Bungeni ambako mambo ya akina sisi petu pakavu hujadiliwa, lugha ya huko ni ya mchaganyiko kimombo na Kiswahili. Hii maana yake nini? Ndiyo, nimesikia, lugha ya kufundishia shuleni toka darasa la tisa na kuendelea huko mbele ni Kiingereza. Sheria zinazomuhusu mwananchi zimeandikwa kizungu. Inaelezwa kwamba toka mahakama ya wilaya hadi mahakama kuu ya rufaa lugha inayotumika huko ni ung'weng'we!

Nimeambiwa kwamba kiongozi yeyote toka China au Japan wanapotayarishiwa dhifa, wao huzungumza kwa lugha ya kwao. Viongozi wetu waendapo Ujerumani au Arabuni wanazungumza Kingereza. Katika mwenendo kama huu, ni kweli lugha yetu tunataka kuienzi na kuwa walezi khasa? Zungumzeni Kiswahili mnapokwenda nje ya nchi. Kingereza sasa hivi kimekuwa ni lugha ya biashara nayo imetanda kotekote. Tunaona haya kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zetu za Afrika! Bali hata ya Afrika Mashariki vilevile wanakwenda wapi waheshimiwa?

Enyi wazungupule, tunayo kazi, tena kazi kubwa sana. Kwa mara nyingine ninaiomba himaya itie nguvu kwa kukitumia Kiswahili katika mahafali yetu yote. Hatuna sababu ya kuazima lugha ya watu wengine. Serikali ivipe uwezo wa hali na mali vyombo vyote vile vinavyoshughulikia lugha yetu ya Kiswahili.. Bakita wanatakiwa wapewe msaada wa kitaalam na fedha. Ukuta wapo hoi wala Serikali haipeleki jicho lake huko. Mambo yataendaje? Himaya ni muhimili mkuu wa lugha yetu vipewe uwezo wa kutosha vile vyombo vinavyohusiana na lugha yetu ya Kiswahili.

Hivi sasa tunavyo vituo kadhaa vya radio na pia yameanzishwa magazeti mengi kwa lugha ya Kiswahili. Ni khatari. Maneno yanayotamkwa kwenye radio hizo na yanayoandikwa katika magazeti hayo ni ya kuboronga Kiswahili. Sijui ni kutoelewa au makusudi! Mtangazaji anasema "Lisaa moja sasa limepita". Mwandishi yu anaandika; "bomba hiyo inatowa sana mimaji"!

Kiswahili Tanzania ndiko kwao, kwa hiyo wakazi wake tunatakiwa kukimanya barabara. Tusipokijuwa vizuri waalimu, watilmidhi wataambuwa nini? Hatujuwi, tujifunze, wakati ni huu. Titi la mama li tamu, lingine halishi hamu.

=Mwisho=

## LUGHA YANGU KISWAHILI

1. Bismillahi awali, Ndiwe Wewe Mhifadhi
   Nipe nguvu ya akili, niseze yanayokidhi
   Uyafanye yawe mali, yeyote yasimuudhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

2. Nakushukuru Jalali, kwa lugha kunikabidhi
   Lugha hii Kiswahili, yenye ladha bila ludhi
   Kuisema, kunakili, kwangu naona faradhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

3. Nakipenda Kiswahili, kwa utamu wa lafudhi
   Kwa kweli nakikubali, na moyoni nakiridhi
   Lugha fasaha kubuli, wala haina gharadhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

4. Nakipenda kwelikweli, sithubutu kubughudhi
   Yangu na ni ya asili, na sasa naihifadhi
   Titi la mamiye mwali, linginewe halikidhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

5. Linginewe uaili, na kwangu lina gharadhi
   Kwenye lisani hudhili, huniletea maudhi
   Hujiuliza maswali, mwenyewe nikawa Kadhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

6. Nitasema Kiswahili, sitakiweka baadhi
   Lugha yangu naijali, siweki utaaradhi
   Naiomba serikali, na waiwekee hadhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

7. Isemwe kila mahali, katika hii ardhi
   Izungumzwe skuli, mahakama kwa Makadhi
   Na waketipo manguli, wa bara letu mafadhi
   Kwani isipate hadhi, lugha yangu Kiswahili.

# Ujumbe wa amani kwa Tanzania

*Kutoka uk. 12*

kuwa ni zenye kipato kikubwa ajabu. Mwandishi fulani wa kimarekani ameandika hivi:

"Kuna idadi kubwa ya watu hapa Marekani wanaotazama sinema kila siku. Kuna mamilioni ya mabinti wafanyao kazi na wanafunzi wanaotazama sinema usiku na mchana. Kwa hakika kuna mamilioni ya watoto na vijana ambao hawajui chochote cha mapenzi, kazi, shughuli za nyumbani, biashara, siasa, ulimwengu au chochote kingine isipokuwa kile wanachoelezwa na sinema hizo.

Kila aina ya dhambi iliyowahi kufanywa na watu wa nabii yeyote aliyepita, inafanywa na kuonyeshwa na sinema hizo, na kusambazwa na kufundishwa duniani kote, kwa mkupuo, kwa njia ya mitandao.

Kiasi kikubwa mno cha fedha kinatumika katika kutimiza ibada za miungu hiyo ya starehe na anasa kwa watu kuzamia ndani ya ulevi, kamari na uasherati, na matokeo yake nyumba nyingi zinabaki zikifilisika, watu wakizama ndani ya madeni, wengi wakibaki wanatota magerezani, wengine wakichukua njia ya mkato ya kujiua, kuyakwepa mateso yasiyovumilika yaliyosababishwa na miungu hiyo ya starehe na anasa. Kwa nini watu wanaendelea kujididimiza ndani ya gharama zote hizi zenye madhara makubwa ya ajabu? Sababu ni kwamba hamu ya starehe hizi huwa haipungui bali huongezeka, mungu bandia wa starehe ni lazima apate hisa yake.

Kama ilivyotokea katika zama za himaya ya Kirumi, ya Pompei, ya Sodom na Gomorrah, ndivyo hivyo inavyotokea leo katika zama zetu hizi. Matendo ya kishetani yaliyowaangamiza wanaume kwa wanawake katika siku za kale, yaliyoteketeza miji na mataifa, yanatendwa bila kificho, kwa mapana na marefu, duniani kote, na kuhamasishwa na hata kushinikizwa na baadhi ya mataifa yenye nguvu duniani kwa vitisho vya kukatiwa misaada.

Ufisadi umekuwa ni ugonjwa ulioenea duniani kote, saratani inayokuwa ndani ya majumba ya kizazi hiki cha mwisho, ikiwaangamiza, ikiwalemaza, ikiwaharibu na kuwavunjia kabisa mipango na matumaini yao. Uovu huu umeenea kiasi hiki kwamba haitakuwa imekosewa kama ikisemwa kuwa, huo ni mpango makhsus wa Ibilis, wa kuiangamiza dunia nzima na kuutokomeza kabisa ustaarabu wetu. Dunia inachupa, bila hiari, kwenye bahari iliyochafuka ya shida na simanzi, ikipigwa na mawimbi makubwa ya tamaa, wakati mawimbi yaendayo kasi ya hofu na ukataji tamaa, yakiivurumisha kuelekea kwenye miamba ya hatari iliyomo ndani ya giza la bahari yenye tufani.

Ingawa Dunia ina kila aina ya uvumbuzi wa sayansi na teknolojia, kila aina ya starehe ya kisasa, kila njia ya kupatia ladha ya kidunia, hakuna yoyote kati ya hizo inayoipunguzia hatari zinazoinyemelea. Watu wenye nguvu wanakwea na kuukamata usukani wa merikebu ya dunia bila ya mafanikio yoyote. Haiwatii tena, meli iko nje ya udhibiti ikitaraji huruma ya upepo na mawimbi yanayoipeleka kwenye maangamio. Mwanadamu hajawahi hapo kabla kuwa katika hali ya kutisha na kukatisha tamaa namna hii. Wanadamu duniani kote wanapiga mayowe ya kupatiwa safina mbadala ya kuwaokoa na tufani hilo. Je, Mungu Mwenye huruma Atawaacha viumbe wake wote wazame ndani ya bahari hiyo ya kutisha?

Hapana! Mungu ni Mwingi wa Huruma na Rehema. Alishatengeneza mazingira kwa wenye kutaka kusalimika. Alishamtuma Nuhu wa zama hizi aliyetengeneza safina ya kuwaokoa wanadamu kutoka kwenye dhoruba hii yenye kutisha mno. Amewatangazia wanadamu duniani kote kwa kuwaambia:

"Mafuriko ya ghadhabu za Mwenyezi Mungu yamefikia kileleni. Wale tu watakaokimbilia ndani ya safina ya Nuhu ndio watakaosalimika. Nitafuteni kwa ukweli na uaminifu wa moyo. Heri imo humu tu. Wanyama wakali wametapakaa kila mahali na ni kwangu tu unakopatikana mnara wa makimbilio wenye salama."

Huyu si mwingine ila ni Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., aliyeitangazia dunia kuwa yeye ndiye yule Masihi na Mahdi na Mujaddid wa karne ya kumi na nne aliyekuwa akisubiriwa sana kudhihiri na kuurekebisha ulimwengu. Ndani ya ukurasa wa 168 wa kitabu chake kiitwacho Kitaabul Bariyya ameandika kwamba:

"Ulipofika mwisho wa karne ya kumi na tatu, na karne ya kumi na nne ilipokaribia kuanza, basi Mwenyezi Mungu Akanipa habari, kwa njia ya Ilhaam (Wahyi), kwamba: wewe ndiye Mujaddid wa karne hii."

Na ndani ya kitabu chake kingine kiitwacho Izaalae awhaam uk. 632, kuna wahyi alioupata toka kwa Mwenyezi Mungu uliosema: yaani tumekufanya wewe kuwa Masihi mwana wa Mariamu.

Akijieleza zaidi Hadhrat Ahmad a.s. anasema ndani ya kitabu chake cha Arbain sehemu ya kwanza uk. 3 kwamba: "Nimefahamishwa kwa Wahyi mtakatifu na uliotakaswa wa Mwenyezi Mungu kwamba mimi nimetoka Kwake nikiwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi wa ahadi, nami nikiwa ni mwamuzi wa hitilafu za nje na ndani. Hili jina langu lililowekwa kuwa Masihi na Mahdi, ni Mtume s.a.w. aliyenipa majina hayo, na halafu, Mwenyezi Mungu, kwa maneno Yake ya moja kwa moja, Amenipa jina hili hili na halafu hali ya sasa ya zama hizi imetaka pia jina langu liwe hili hili."

Hadhrat Ahmad a.s. alidhihiri katika mji mdogo wa Qadian huko India na kutimiza bishara za manabii kadhaa waliopita waliobashiri kuwa Nabii wa zama za mwisho atadhihiri katika sehemu hiyo ya Mashariki ya dunia.

Siku moja Mtume s.a.w. alisema kwamba Imam Mahdi atatokea katika eneo liitwalo Kaadiah (Qadian). Hii Hadithi yapatikana ndani ya kitabu kilichoandikwa mnamo mwaka wa 840 Hijriyya, yaani zaidi ya karne tatu kabla ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, kiitwacho Jawaahirul Asraar cha Hadhrat Sheikh Ali Hamza bin Ali Malik Twausii isemayo;

Mahdi atatokea katika eneo litakaloitwa Kaadiah na Mwenyezi Mungu Atamsadikisha. Atawakusanya masahaba zake wa nchi za mbali katika idadi ya watu wa Badri, watu mia tatu kumi na tatu.

Ndani ya kitabu kitakatifu cha dini ya Kihindu kuna bishara isemayo:

"Kuna mtakatifu fulani atadhihiri na kuonyesha ushujaa wake katika sehemu iitwayo Qadun." ambayo kwa hakika ndio Qadian. (Athar ved, kand ya 20, saukat ya 97, mantar ya 3).

Halikadhalika ndani ya kitabu cha Masingasinga cha Janam Saaki bhai bhala waali waddii saaki uk. 251 kuna riwaya isemayo kwamba Bwana Mardane alimuuliza hivi Guru Nanak:

"Guru sahib! Je kutakuwepo na Guru mwingine atakayekuwa mtakatifu zaidi kuliko Kabir Bhagat? Kama atakuwepo ni wapi na lini?" Hapo Guru Nanak akasema: "Guru ajaye atakuja miaka 100 baada yetu, atakuwa ni mmiliki wa ardhi na atatokea katika maeneo ya Batala." Qadian imo ndani ya eneo miliki la Batala.

Yesu pia alisema kuwa atatokea Mashariki kama alivyosema: "Kwa maana, kama vile umeme utokavyo Mashariki na kuonekana hata Magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake mwana wa Adam." Yesu aliitoa bishara hii wakati akiwa Jerusalem. Na Qadian, mji aliozaliwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., uko upande wa mashariki wa Jerusalem.

Hata Mtume Muhammad s.a.w. alisema kuwa Masihi Isa bin Mariam ataibukia kwenye mnara mweupe uliopo Mashariki ya Damascus. [Ibni Maajah]. Ukiitazama ramani utaiona Qadian ikiwa upande wa Mashariki kabisa wa Damascus.

Imam Bukhari ameandika ndani ya kitabu chake cha Historia kwamba Hadhrat Anas bin Malik r.a. alisimulia kwamba siku moja Mtume s.a.w. alisema kwamba "kutakuwepo na kundi litakalopigana vita ya Jihadi huko India, nalo litakuwa pamoja na Imam Mahdi ambaye jina lake litakuwa ni Ahmad."

Halafu ndani ya kitabu cha Bihaarul Anwaar jal. 13 na Abuu Daud jalada la 2 bab khurujul Mahdi, na hata ndani ya Ibnu Maajah, Mtume s.a.w. amenukuliwa akisema kuwa: "Watu watatokea Mashariki watakaotoa taarifa kuhusiana na Mahdi ambaye ndiye atakayekuwa kiongozi wao." Yaani watamuunga mkono na kumsaidia.

Bishara hizi za manabii mbali mbali waliopita katika zama na maeneo tofauti, ziliandaliwa kuja kuwaongoza watu wa dini tofauti, wa zama zetu hizi, kumtambua mwokozi wetu wa kuja kutuingiza katika amani na upendo. Mwenyezi Mungu Alimfunulia Mwokozi huyo, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., habari nyingi za mambo yatakayotokea baadae, yakiwemo ya majanga yatakayoisibu dunia yetu ya leo.

Katika wakati wake hakukuwa na nchi yoyote ya Mashariki iliyoweza kukabiliana na nchi zenye nguvu za Magharibi. Lakini mnamo mwaka 1904, alifunuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa nchi fulani za Mashariki zitaibuka na kuwa nchi zenye nguvu na kuweza kukabiliana na nchi zenye nguvu za Magharibi. Haukupita muda mrefu baada ya kutolewa bishara hii, nchi ya Mashariki ya Japan ikaishinda Urusi katika vita na kuwa miongoni mwa nchi zenye nguvu duniani.

Japan nayo ikashindwa katika vita kuu ya pili ya dunia na China ikaibuka kuwa miongoni mwa nchi za Mashariki yenye nguvu duniani. Kuibuka kuwa mataifa yenye nguvu kwa mataifa haya mawili ya kimashariki, kukabadili mwelekeo wa historia na athari zake zimeendelea kuenea duniani kote, na leo hii China na Japan ni nchi tajiri sana na zenye nguvu kubwa duniani.

Mnamo mwaka 1905, Hadhrat Ahmad a.s. alipata ufunuo mwingine uliofahamisha kuwa Kaisari wa Urusi pamoja na familia yake na serikali yake yote itakumbwa na msiba na madhila makubwa sana na kuangamizwa kabisa. Ni ajabu kwamba ndani ya miezi michache tu kikaundwa chama cha siasa huko Urusi kilichokuja kuuangamiza kabisa utawala wa mfalme Kaisari wa Urusi miaka 12 au 13 baadae. Chama cha kikomunisti kikashika hatamu na kumng'oa Mfalme wa Urusi na hatimaye kumuua baada ya kumdhalilisha mno pamwe na familia yake.

Ilibashiriwa na mitume waliopita kuwa katika siku zetu hizi za mwisho wa dunia, wakati wa kudhihiri Imam Mahdi a.s., dunia itagawanyika katika makundi mawili yenye kuhasimiana. Yatakuwa ni mataifa yenye nguvu sana kiasi ya kwamba hakuna Taifa lolote litakaloweza kupambana nayo. Hatimae, mataifa hayo ya Magharibi na Mashariki, yatapigana vita na kuangamia.

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Imam Mahdi, Mirza Ghulam Ahmad a.s., alifahamishwa na Mwenyezi Mungu na kuutangazia ulimwengu kuwa vitatokea vita vikuu vitano vya dunia. Kuhusiana na vita kuu ya kwanza ya dunia alitangaza kwamba itakuwa ni vita itakayotokea kwa ghafla mno kiasi ya kuishangaza dunia. Alibashiri kuwa watakaokutwa na vita hiyo wakiwa safarini watapata shida mno, mito itageuka myekundu kwa damu, vijana wataonekana kama wazee kutokana na shida na misukosuko ya vita hiyo, milima italipuka, watu watawehuka kutokana na hofu ya vita, na huo utakuwa ndio wakati wa kuangamia kwa Kaisari wa Urusi, mbegu za ukomunisti zitapandwa wakati huo, manowari za kivita zitawekwa katika hali ya tahadhari, vita kubwa ya baharini itapiganwa, falme zitapinduliwa na miji itageuka kuwa makaburi. Vita hii ikaja tokea miaka sita baada ya Hadhrat Ahmad a.s. kufariki, kwani alimwomba dua Mwenyezi Mungu kuwa Amfishe kabla ya kutokea kwa vita hiyo. Hayo yote yaliyotabiriwa naye yakatokea vivyo hivyo.

Pia alitabiri janga lingine kwa sura ya vita kuu ya pili ya dunia itakayokuwa ni kubwa na yenye maafa zaidi kuliko ile ya kwanza. Vita itakayoibadili ramani ya dunia na kubadili mwelekeo wa watu. Ukomyunisti ulitabiriwa kupata nguvu wakati huo na kuwa taifa lenye kuogopeka, mataifa mengi yatakuwa chini ya himaya yake.

Na ndivyo ilivyotokea, kwani baada ya vita kuu ya pili ya dunia, nchi nyingi za Ulaya ya Mashariki zikawa za Kijamaa na kufuatiwa na watu milioni mia saba wa China na nchi nyingi za Ulimwengu wa tatu zikiwemo za Afrika, Asia na za Amerika ya Kusini. Hapo Dunia ikagawanyika katika kambi mbili zenye uadui na silaha za kutisha.

***Itaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Mshairi aandika juu ya Mshairi

*Kutoka uk.12*

tuvu na tamakuni na vijana wote wa Sheikh Amri waliushangilia na wakakubali mswada huo uchapishwe katika sura ya kitabu. Watoto wa pande mbili walikubaliana kisibadilishwe chochote katika mswada huo.

Baada ya makubaliano hayo, tatizo la fedha za kuchapisha kitabu hicho ilijitokeza. Habari hizo zilimfikia Bwana Mohamedi Iqbal Dar aliyemfahamu vilivyo Sheikh Amri. Yeye akakubali kugharamia fedha zote za uchapishaji. Itakumbukwa ya kwamba Bwana Dar ni yule aliyebuni jina Tanzania, na ndiye aliyelipa gharama za kitabu cha *Almasi ya Afrika* kinachoeleza maisha ya Sheikh Amri kilichoandikwa na mwanae wa pili Sheikh Bakri Kaluta. Ni Bwana huyu pia aliyegharamia kitabu cha *Nani aliyebuni jina Tanzania?* Kazi ya kuchapisha kitabu walipewa Ahmadiyya Printing Press - Kampuni ya uchapishaji inayoendeshwa na Jumuiyya ya Ahmadiyya katika Tanzania.

Kufanikisha harakati za kuchapisha mswada huu iliundwa kamati. Bwana Amiri Abedi na Mahmood Hamsin Mubiru walikwenda kwa Dr. Ahmad Kiwanuka ili kuomba ushauri wake juu ya uchapishaji wa mswada huu. Dr. Kiwanuka ni msomi ambae amepitia maandiko mengi ya Sheikh Kaluta Amri Abedi na aliwahi kuniambia kwamba viongozi wetu walipewa vipaji maalum, na akasema kazi zote hizi nzito Sheikh Amri alizifanya bado ni kijana, kwani alifariki mwaka 1964 akiwa na umri wa miaka 40. Dr. Kiwanuka alianiambia kwamba Mwalimu Nyerere siku zote alikuwa akisema ya kwamba alikuwa na wataalamu wawili na wote kutoka Kigoma. Wataalamu hao ni Sheikh Kaluta Amri Abedi ambaye Nyerere alimwita mtaalamu wa Kiswahili na Godwin Tunze mtaalamu wa Kiingereza.

Dr. Kiwanuka alitupa ushauri mwema, wa kuonana na balozi Jaafari Msolomi kwani Bw. Msolomi alifahamiana vilivyo na Sheikh Amri na alipotoka masomoni Pakistani Bw. Jaafari Msolomi alikaaa nyumbani kwa Sheikh Amri mtaa wa Shaabani Robert, mtaa ulio karibu na Ikulu ya Dar es salaam. Balozi Msolomi kwa moyo mkunjufu alitukaribisha nyumbani na kukubali jukumu la kushughulikia suala hili. Balozi Jaafari Msolomi kama tulivyokwisha sema, alisomea Pakistani na kufanya kazi wizara ya mambo ya nchi za nje na kwa miaka 6 alikuwa balozi wa Tanzania huko Guinea ya Rais Ahmad Sekuture. Ni mtunzi mzuri wa mashairi na moja ya ubingwa wake unajitokeza alipoweza kutafsiri kutoka Kiingereza utenzi juu ya maisha ya Mtukufu Mtume Muhamamd (saw) ulioandikwa na muanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya duniani - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Beti mbili za mwanzoni zinasema:-

Muhammad Muungamu, wewe ndiye wetu chemu chemu

Ya rehema za Karimu, kama maji baharini

Bahari isokauka, ya fadhila za rabuka

Makundi yaja haraka, kujitwalia vyomboni.

Balozi Msolomi alishauri kuimarisha kamati hiyo kwa kupendekeza Mshairi Amir Sudi Andanenga, Suleimani Hega na Brigedia Generali Hashim Mbita waingizwe kwenye kamati hii.

Mshairi Amiri Sudi Andanenga alifahamiana vizuri na Sheikh Amri na aliwahi kumpa ari ya kuendelea kutunga mashairi. Baadhi ya mashairi ya Sheikh Amri Bwana Andanenga ameyahifadhi kwa ghaibu. Suleiman Hega ni mtangazaji maarufu na umaarufu wake ulifurutuada katika kipindi cha mbinu za Kiswahili. Akiwa mwana Dar es salaam alikutana mara kwa mara na Sheikh Amri aliyekuwa Mbashiri wa Ahmadiyya katika jiji la Dar es salaam. Brigedia Generali Hashim Mbita alikuwa afisa wa habari wa Mkoa wa Tabora ambako Sheikh Amri alikuwa Mkuu wa Mkoa. Brigedia Mbita aliwahi pia kuwa Mwandishi wa habari wa Mwalimu Nyerere kabla ya kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa kamati ya ukombozi wa Afrika. Kazi aliyoifanya ni kubwa ambayo imekamilisha ukombozi wa Afrika, ingawaje uhuru wenyewe bado ni uhuru wa bendera!

Kamati ilianza kukaa kwa Brigedia Generali Hashim Mbita, sehemu za Chang'ombe jijini Dar es salaam. Shabaha ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kumpata Rais wa Jamhuri ya Muugnano wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete ili awe mgeni rasmi katika uzinduzi wa kitabu hicho. Jitihada kubwa zilifanywa zikiwemo na za kufahamiana naye. Matumaini yalikuwepo lakini mara yakatoweka kabisa. Matumaini yalipokwisha ikaonelewa ya kwamba atafutwe mtu mwingine, kwani Waswahili husema; "Kuadimika kwa wali hakuna kisicholika".

Jitihada zilifanyika na hatimaye akapatikana Kingunge Ngombare Mwiru. Komredi Kingunge katika siasa za Tanzania ananasibishwa na siasa ya ujamaa. Ni hodari katika kuielezea nadharia ya ujamaa na kalamu yake haioneshi kuishiwa na wino katika kuitetea nadharia ya ujamaa. Katika kufafanua ujamaa wa Tanzania sidhani kama kuna anayemkaribia Kingunge kwa ufasaha na uwezo wa kuweka nadharia ya ujamaa bayana. Kupatikana kwa Kingunge kuliipa sana faraja Kamati. Kamati ilimteua balozi Job Lusinde kuwa mwenyekiti wa uzinduzi huo wa kitabu cha historia ya maisha ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Balozi Job Lusinde ni Mwalimu aliyewahi kufundisha shule ya Dodoma Aliance. Kutoka hapo alijihusisha na harakati za ukombozi na wakati wa uhuru alikuwa miongoni mwa Mawaziri wa mwanzoni. Wakati Sheikh Kaluta Amri Abedi akikabidhiwa hati za kufanya mji wa Dar es salaam kuwa jiji katika viwanja vya Karimjee na Mme wa Malikia Elizabeth, Job Lusinde alikuwa Waziri wa Serikali za Mitaa. Baadae alipelekwa Kenya ambapo alikuwa Balozi wa Tanzania katika nchi hiyo kwa miaka mingi. Sifa zake za ukarimu na kupenda kukaribisha wageni zimetolewa ushahidi na Watanzania wengi walioenda Kenya kwa shughuli zao binafsi, kufundisha au kusoma.

# Mahubiri yapambamoto chuo kikuu cha WaislamuMorogoro

kutualika tena siku nyingine. Maandalizi ya mtihani wa kumaliza muhula yaliwafanya wakose muda wa kutualika tena hadi wanakwenda likizo.

Mwezi Machi chuo kilipofunguliwa Mwenyekiti bwana Adam alinieleza kuwa wanatuhitaji tena. Alinidokeza kuwa baadhi ya wanafunzi wanaomba nisiende na Sheikh wakidai ni maji marefu na si saizi yao. Nilimfahamisha kuwa nitakwenda nae na kumwambia kuwa wanaotoa hoja hizo ni wapenda ubishi na si watafuta elimu.

Nilienda na Sheikh kwa mara nyingine katika hostel za cheers na kufanya mazungumzo na wanafunzi hao. Baadhi ya wanafunzi waligoma kutokea kutokana na ujio wa Sheikh lakini mazungumzo yaliendelea kama kawaida. Siku hiyo hali ilikuwa tofauti kwani ulizuka mjadala mzito kutoka katika sura 61:7 na kuchukua muda mrefu hadi mwisho wa mazungumzo. Kutokana na Mtume aliyetajwa katika aya hiyo wao walidai ni Muhammmad na si mwingine. Sheikh alipangua hoja yao kwa kumalizia aya ya nane ya sura hiyo inayosema kuwa sifa ya nabii huyo ataitwa ndani ya uislamu, sifa ambayo Mtume Muhammad (s.w.a) hana. Kujitoa katika kigingi hicho walihoji je, baada ya Issa alikuja Ahmad au Muhammad?

Sheikh aliwapa mfano katika sura 46:31 kutengua hoja yao, ndipo baadhi yao wakataka kuvunja mazungumzo lakini wenzao waliwapuuza na kuwazuia hali iliyofanya mazugumzo yaendelee. Muda wa magharibi ulipokaribia mwenyekiti alisitisha kikao huku wengi ao wakiwa bado wana shauku ya kuuliza maswali. Kuna baadhi ya watu walijaribu kuzuia mazungumzo hayo wakidai mwenye hosteli hajaruhusu. Kwa hamasa ya kutafuta elimu wanafunzi walihoji, mbona mabishano ya soka huwa hayazuiliwi sembuse mazungumzo ambayo jina la Mwenyezi Mungu na Mtume wake linatajwa.

Kiu ya kujua zaidi juu ya Ahmadiyya ilizidi kushika kasi miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro. Hoja juu ya utume kuendelea na kifo cha Nabii Issa (as) zilipata mashiko makubwa miongoni mwao. Hali hiyo iliwapelekea kila wanaponiona kunihoji juu ya masuala mbalimbali ya dini katika msimamo wa kiahmadiyya. Nililazimika kutumia muda mwingi nikiwa chuoni kuhubiri. Hali hiyo ilipelekea nipewe majina mbalimbali na wanafunzi wenzangu chuoni kama vile; Ahmadi Mirza, Qadiani, Ahmadiyya n.k. Wapo waliyokuwa wakinidhihaki ya kwamba nalipwa fedha na wahindi kwa kufanya kazi hiyo. Wengine wakahukumu dini ya Kiislamu makao yake makuu hayawezi kuwa Uingereza,ilimradi tu walikosa hoja za msingi.

Majadiliano ya juu ya hoja mbali mbali za kiahmadiyya yakachukua sura mpya katika kijiwe cha siasa kilichopo karibu na geti kuu la Chuo hiki ambacho ni pekee cha Waislamu hapa nchini kilichosheheni wasomi kutoka maeneo mbalimbali duniani. Kijiwe hicho ambacho inaaminika kuhudhuria hapo ni zaidi ya shahada, kina kusanya wanafunzi wengi wanaosifika katika kutafakari mambo kwa kina. Hivi karibuni kimebatizwa jina na kuitwa kijiwe cha wanaharakati. Mtu yeyote chuoni hapo anayejitambulisha kuwa mwanaharakati na si mwanachama wa kijiwe hicho watu humuona kama kioja.

Majadiliano marefu baina yao yaliwafanya wapate hamu ya kutembelewa na Sheikh wa kiahmadiyya ili awatoe uvulivuli na ukakasi juu ya masuala waliyokuwa wana shaka nayo. Tarehe 10/04/2013 mnamo majira ya saa kumi na nusu ujumbe wa Ahmadiyya ukiongozwa na Sheikh Bakri uliwasili katika kijiwe cha wanaharakati hatua chache kutoka geti kuu la chuo.

Baadayasalamunautambulisho, mazungumzo yalianza rasmi chini ya Mwenyekiti Halfani Mshana mwanafunzi wa mwaka wa pili katika shahada ya kwanza ya sanaa na ualimu. Alhaji Sheikh Bakri Kaluta alipewa nafasi kueleza kwa ufupi juu ya Ahmadiyya. Baada ya maelezo mafupi ya Sheikh wanafunzi walipata fursa ya kuuliza maswali na Sheikh aliwajibu kwa ustadi mkubwa kwa kuzingatia kiwango cha elimu yao. Alitoa ushahidi wa hoja na dalili kutoka katika Qur'ani Tukufu na hadithi za Mtume Muhammad (saw). Maswali mengi yalizama katika yakini ya Seydna Ahmad (a.s) yaani kuendelea kwa utume na kifo cha Nabii Issa (a.s).

Saa kumi na mbili na nusu jioni Mwenyekiti aliahirisha kikao akiwaomba wanafunzi wenzake wakajipange kwa kutafuta ushahidi wa kutosha juu ya hoja wanazozipinga. Wote walikubaliana na rai ya Mwenyekiti wakaahidi watakapokuwa tayari watatualika tena. Alhaji Sheikh Bakri Kaluta aliwasihi kuacha ushabiki na jazba katika kusoma masuala ya dini na badala yake kutafakari ukweli kwa hoja na dalili. Pia Sheikh aliwaalika ofisini kwake wakati wowote watakapopata wasaaa wa kufanya hvyo.

Pamoja na Alhaji Shekh Bakri ujumbe wa Ahmadiyya ulikuwa na watu watano.Wengine ni bwana Nasiri Mnungu, Hamisi Madua, Hamidu Salehe, Maliki Ramadhani na Lutufu Mbanga ambaye ndiye mwandishi wa habari hizi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie ujumbe wa Masihi ufike ndani kabisa ya chuo utakase nyoyo zao na kuzaa matunda yaliyo mema. Amin.

## KUMRADHI

**Katika toleo lililopita, makala mbili : '*Ujumbe wa amani kwa Tanzania*' na '*Mahubiri yapambamoto chuo kikuu cha Waislamu Morogoro*', zilichanganyika na hivyo kuleta mkanganyiko mkubwa miongoni mwa wasomaji wetu.**

**Kwa sababu hiyo makala hizo zimerejewa tena katika gazeti hili.**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza.**

***Mhariri***

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# MapenziyaMungu

Rajab 1434 AH | Mei 2013 | Hijrat 1392 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

**Imesimuliwa na Hadhrat Uthman bin Affaan r.a. ya kwamba yeye alimsikia Mjumbe wa Allah s.a.w. akisema: Yule anayejenga msikiti kwa ajili ya Mungu, Mwenyezi Mungu Atamjengea (nyumba) mfano wake katika Pepo. (*Muslim*)**

# Ujumbe wa amani kwa Tanzania

**Hotuba iliyotolewa na Sheikh Bakri Kaluta katika mkutano wa amani - Morogoro 2013**

Mungu ni Upendo, Mungu ni Amani, Upendo hauwezi kuzaa chuki, na Amani haiwezi kuelekeza kwenye vita. Ndio sababu kauli mbiu ya Jumuiya yetu imedumu kuwa Upendo kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Leo dunia inapigwa na bumbuazi kwamba ni nini kimeikumba jamii yetu kiasi ya kwamba upendo na amani vinatoweka kwa kasi miongoni mwetu na hatimae kuibuka chuki inayoelekeza kwenye vita. Ni nini kimesababisha hali hii. Majibu tofauti yanatolewa na jamii mbali mbali, kila mmoja katika anga zake. Hebu tuizamie kwa kina hali hii tujaribu kuibuka na sababu zenye thamani zitakazoweza kuinusuru jamii yetu ya Tanzania, Afrika na dunia nzima.



*Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood (wa pili kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na wabashiri wa Mkoa wa Morogoro wakati wa Mkutano wa amani uliofanyika tarehe 7/4/2013. Wa mwanzo kushoto ni Sheikh Bakri Kaluta - mwandishi wa makala hii.*

Hakuna shaka kwamba mwanadamu ameshindwa kuidhibiti tamaa ya kuziabudu kazi alizozitengeneza kwa mikono yake mwenyewe, na amempuuza Mungu Yule ambaye msukumo wa mafanikio yote huchimbukia Kwake. Chini ya shinikizo la kuyahangaikia maisha ya kisasa yanayoboreshwa na kurembeshwa kiajabu kutokana na elimu ya Sayansi na Teknolojia, wazo la Mwenyezi Mungu limetoweka kabisa ndani ya akili za watu wengi sana, ni sawa tu na kusema kuwa wazo la Mwenyezi Mungu halipo kabisa ndani ya akili zao.

Mungu bandia wa dhahabu amepata wafuasi wake walio waaminifu kabisa, Tamaa imedumu kupata wafuasi wengi wa kumuabudu kwenye hekalu lake. Takriban dunia nzima imeinama kwa heshima na taadhima mbele ya mungu bandia wa ulafi, umero na uchoyo.

Kamari, kama vile alivyo mungu mammon, mungu bandia wa ulafi, umero na uchoyo, ni mungu wa majonzi na simanzi. Imeziangamiza nyumba zisizo na idadi. Kila siku kamari inatoa matumaini ya uongo ya kuneemeka kiulaini ndani ya mioyo isiyo na idadi, na hatimaye kuwatumbukiza, bila huruma, ndani ya mashimo marefu ya majonzi. Inadhoofisha nguvu kazi, inaiharibu juhudi ya kweli, inazalisha hali ya kutotosheka, ya kukata tamaa na ya kuvunja moyo. Hizi ni hali zenye kuufukuza upendo na kuikaribisha chuki isiyovumilia hata kidogo manukato ya amani, bali ni yenye kuvutiwa mno na harufu itishayo ya damu.

Mungu mwingine wa bandia anayeabudiwa siku hizi ni mungu wa starehe na anasa anayesababisha shughuli za mambo haya ya starehe na anasa

*Endelea uk. 10*

# Mahubiri yapambamoto chuo kikuu cha Waislamu Morogoro

*Na Lutufu A. Mbanga - Morogoro*

Mjadala wa kihistoria ilibidi ufanyike mwaka jana mwanzoni katika Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro baina ya Sheikh ambaye ni mwanafunzi wa chuo hicho dhidi ya Waahmadiyya. Kutokana na sababu mbalimbali mjadala huo ulishindikana kufanyika. Moja ya sababu kubwa ikiwa kutoonekana kwa Sheikh ambapo hata alipotafutwa kwenye simu yake hakupatikana.

Kushindikana kwa mjadala huo haukuwa mwisho wa harakati za mahubiri katika chuo hicho zilizokuwa chini ya Majlis Khudamul –Ahmadiyya Morogoro mjini. Kutokana na mazungumzo ya kidini kati ya mwandishi wa habari hizi na wanafunzi wenzake chuoni hapo, wanafunzi hao walishikwa na shauku kubwa ya kufahamu zaidi juu ya Ahmadiyya. Miongoni mwa hoja zilizoteka hadhira kubwa miongoni mwao ni juu ya utume kuendelea na kifo cha Nabii Issa (a.s).

Shauku ya wanafunzi hao ilienda sambamba na haja ya Alhaji Sheikh Bakri Kaluta ya kufikisha ujumbe wa Masihi



*Mwalimu Lutufu Abdallah Mbanga, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro.*

katika kila kona. Nilipofika Morogoro Oktoba 2011 kuanza masomo yangu chuoni hapo, Alhaji Sheikh Bakri alinitaka nijitahidi kadri ya uwezo wangu ujumbe wa Masihi ufike chuoni hapo. Aliniahidi wakati wowote atakapohitajika yupo tayari kufika ili kutimiza ile bishara aliyopewa Seydna Ahmad na Mwenyezi Mungu ya kwamba "Nitafikisha ujumbe wako katika kila pembe ya dunia".

Mnamo Januari mwishoni, majira ya saa kumi kasoro alasiri nilipokea simu kutoka kwa mwanafunzi Ramadhani Bhatia, anaeishi hosteli za cheers zilizo nje kidogo ya chuo. Alinieleza ya kwamba wananihitaji kwa ajili ya kupata ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali za kiahmadiyya. Nilifika msikitini kwa ajili ya sala ya alasiri na baada ya sala nilimueleza Sheikh juu ya haja ya wanafunzi hao na kumuomba tuongozane pamoja. Sheikh alithibitisha kauli yake kwa vitendo. Kwa bashasha na furaha iliyozidi kifani alifunga ofisi tukaaongozana hadi hostel za cheers.

Mazungumzo yaliyokuwa yakiongozwa na mwanafunzi mwenzao bwana Adam, yalikuwa mazuri na kuvuta hisia za pande zote mbili. Sheikh alipewa nafasi ya kueleza kwa muhtasari juu ya historia ya Ahmadiyya na shabaha ya kuanzishwa kwake. Baada ya maelezo ya Sheikh wanafunzi walianza kuuliza maswali, ambayo sheikh aliyajibu kwa hoja na dalili kutoka katika Qur'an Tukufu na hadith za Mtume Muhammad (s.a.w). Kama ilivyo kawaida maswali mengi yalijikita katika utume kuendelea na kifo cha Nabii Issa (a.s). Ilipofika majira ya saa kumi na mbili na nusu jioni mwenyekiti alisitisha mazungumzo hayo na kutuahidi watajipanga na

*Endelea uk. 11*

# Mshairi aandika juu ya Mshairi

**Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es Salaam**

Ukumbi wa Karimjee ulioko jijini Dar es salaam una nafasi maalum katika taarikh ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Ni katika ukumbi huu ndipo sauti ya Mbunge wa Kigoma wa siku hizo Sheikh Kaluta Amri Abedi aliposikika akitoa wito wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya Taifa la Tanganyika. Ni katika ukumbi huo huo ndipo kilio hicho cha Sheikh Kaluta Amri Abedi kilipotekelezwa kwa vitendo wakati Julius Kambarage Nyerere kiongozi wa Tanganyika katika mwaka 1962 alipohutubia Bunge kwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiswahili.

Katika ukumbi huo huo tarehe 12/03/2013 palifanyika dhifa ya kisomi ya aina yake iliyohusu uzinduzi wa kitabu juu ya maisha ya mtu maarufu katika ulimwengu wa Kiswahili Sheikh Kaluta Amri Abedi na kilichoandikwa na muandishi mahiri Bw. Mathias Mnyampala kiitwacho '*Maisha ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi*'.

Mwaka 2000 mwana wa pili wa Bwana Mathias Mnyampala Charles alifunga safari ya kutoka Dodoma hadi Dar es salaam. Madhumuni ya safari hii ilikuwa ni kuwatafuta watoto wa Sheikh Kaluta Amri Abedi kwani alikuwa ana hazina iliyoachwa na baba yake. Toka baba yake afariki mwaka 1969 Charles aliendelea kuitunza miswaada ya maandishi ya Bwana Mathias Mnyampala ambayo ilikuwa bado haijachapwa. Ulikuwa ni wakati mgumu kwa kijana huyu aliyeonyesha mapenzi makubwa kwa baba yake. Alijitahidi kupeleka miswada hiyo katika makampuni kadhaa ya uchapishaji hadi Chuo kikuu cha Dar es Salaam katika taasisi inayohusika na utafiti wa Lugha ya Kiswahili, kote huko aligonga mwamba.

Kama Karama katika riwaya ya Shaabani Robert - *Kusadikika*, Charles hakukata tamaa. Kila alipohama, alihama na miswada hiyo. Kuna wakati nyumba aliyokuwa anaishi ilikumbwa na mafuriko, yeye aliacha vitu vyote na kuogelea kuokoa miswada hiyo.

Kwa sudi ya ajabu alipata wazo la kuwatafuta watoto wa Sheikh Amri. Aliuliza sana na msamaria mwema mmoja alimueleza njia rahisi ni kufika Msikiti wa Ahmadiyya ulio Mnazi Mmoja jijini Dar es salaam hapo muulizie Bwana mmoja anaitwa Mahmood Hamsin Mubiri huyu ameandika sana juu ya maisha ya Sheikh Amri na pia ni mkwe wake, bila shaka utawapata watoto hao.

Charles alifanya hivyo na Mungu bariki watoto wa Sheikh Amri wakakutana na watoto wa Bwana Mathias Mnyampala. Charles aliwaonyesha watoto wa Sheikh Amri mswada wa Bwana Mathias Mnyampala juu ya maisha ya Sheikh Amri. Mswada huo ulisomwa kwa

*Endelea uk.11*